# KANISA LA METHODIST TANZANIA

# (MCT)

# KANUNI ZA UENDESHAJI WA KANISA LA METHODIST TANZANIA

## TOLEO LA KWANZA MWAKA 2024

## YALIYOMO


**UTANGULIZI:**

**SEHEMU YA KWANZA: UFAFANUZI**

IBARA YA 1: TAFSIRI YA MANENO

IBARA YA 2: MAMLAKA YA KUTOA TAFSIRI

**SEHEMU YA PILI: UTAMBULISHO WA KANISA**

IBARA YA 3: JINA LA KANISA

IBARA YA 4: MAKAO MAKUU

IBARA YA 5: NEMBO YA KANISA

**SEHEMU YA TATU: MAONO UTUME NA MALENGO**

IBARA YA 6: MAONO YA KANISA

IBARA YA 7: UTUME WA KANISA

IBARA 8: MALENGO YA KANISA

IBARA YA 9: IMANI YA KANISA

**SEHEMU YA NNE: WASHIRIKA NA WAKRISTO**

IBARA YA 10: WASHIRIKA

IBARA YA 11: WAKRISTO

**SEHEMU YA TANO: UONGOZI**

IBARA YA 12: VIONGOZI WA KANISA

IBARA YA 13: UTUMISHI NDANI YA KANISA

IBARA YA 14: HAKI NA TARATIBU ZA UTUMISHI

IBARA YA 15: BODI YA WADHAMKINI WA MALI ZA KANISA

## SEHEMU YA SITA: UTARATIBU WA UCHAGUZI NA AJIRA

IBARA YA 16: ASKOFU MKUU

IBARA YA 17: ASKOFU WA SINODI

IBARA YA 18: MCHUNGAJI KIONGOZI

IBARA YA 19: MCHUNGAJI

IBARA YA 20: MWINJILISTI

IBARA YA 21: MZEE WA KANISA

IBARA YA 22: SHEMASI

## SEHEMU YA SABA: MABARAZA, KURUGENZI NA IDARA

IBARA YA 23: MKUTANO MKUU WA KONFERENSI

IBARA YA 24: KAMATI TENDAJI YA KONFERENSI

IBARA YA 25: BARAZA LA MAASKOFU

IBARA YA 26: MKUTANO MKUU WA SINODI

IBARA YA 27: KAMATI TENDAJI YA SINODI

IBARA YA 28: BARAZA LA SAKETI

IBARA YA 29: BARAZA LA KANISA LA MAHALI

IBARA YA 30: IDARA YA HUDUMA ZA KIROHO

IBARA YA 31: IDARA YA HUDUMA ZA JAMII

IBARA YA 32: IDARA YA KURUGENZI YA MIPANGO, UCHUMI, UWEKEZAJI NA MAENDELEO

IBARA YA 33: KURUGENZI YA RASILIMALI WATU UTAWALA NA UONGOZI

**SEHEMU YA TISA: NDOA**

IBARA YA 35: NDOA ZA KIKRISTO

**SEHEMEU YA KUMI: KUTATUA MGOGORO**

IBARA YA 36: TARATIBU ZA KUTATUA MGOGORO

IBARA YA 37: KUSIMAMISHWA NA KUONDOLEWA KATIKA UTUMISHI

**SEHEMU YA KUMI NA MOJA: MAREKEBISHO YA KANUNI NA KATIBA**

IBARA YA 38: SABABU YA KUREKEBISHA KANUNI/KATIBA

IBARA YA 39: UTEUZI WA WAJUMBE WA KAMATI YA KANUNI NA KATIBA

**SEHEMU NA MBILI: KUVUNJWA KWA KANISA**

IBARA YA 40: UTARATIBU WA KUVUNJWA KANISA

**SEHEMU YA KUMI NA TATU: MENGINEYO**

IBARA YA 41: MUUNDO WA MCT

**SEHEMU YA KUMI NA NNE: MAAFIKIANO**

IBARA YA 42: MAAFIKIANO

## UTANGULIZI

Kanisa ni chombo cha pekee ambacho kiko chini ya Bwana mmoja yaani Yesu Kristo.Neno hili limetokana na neno la Kiyunani Eklesia ambalo matumizi ya kawaida kwa jamii ya wakati ule wa kale kumaanisha mkusanyiko wa watu wenye nia fulani aidha ya kidini; kisiasa au ya kimaendeleo.Ili kutofautisha hili na lile la kawaida la kijamii wafuasi wa Yesu walitumia maneno **Eklesia tou theu** kumaanisha ili ni kusanyiko la watu wa Mungu yaani kanisa.

Kanisa popote linabeba sura mbili zinazoachana yaani mwili na Taasisi inayoshikamana na Yesu Kristo katika utendaji wake mara sura mbili zinapokuwepo basi haja ya kuwepo miongozo ya kiutendaji uhitajika Sana na hii inasababisha kutayarisha kanuni za kuliongoza kanisa la Methodist Tanzania – (MCT) katika utendaji wa kila siku, kwa mabaya kufafanua katiba.

Kwa hiyo kila mkristo anaelekezwa kuwa mtiifu na mnyenyekevu kwa Yesu Kristo na Kanisa lake kufuata taratibu za maisha ya Kikristo na huduma za Kiroho kwa Uaminifu. Kanuni hizi zinalinda nidhamu ya maisha yetu na kutulinda katika utekelezaji, kusudi tusikiuke utaratibu na kuvunja umoja na ufanisi tunaoutegemea. Ni tumaini kuu la kanisa kuwa kila muumini wa kanisa la Methodist (MCT) atafuata kanuni hizi ; kwa moyo wote mbele za Mungu ili kuhifadhi na kudumisha Amani ,Umoja,Ushuhuda na heshima kwa kazi za kanisa.

Aidha kanisa ni Taasisi ya kiroho inayojiendesha shughuli zake kwa kutegemea michango, Zaka, Matoleo ya waumini na washiriki wa ndani na nje ya nchi; Uchumi wake unategemea waumini na washiriki wanaotoa kwa hiari yao ingawa ni wajibu wao kibiblia.Kwa hiyo kanisa wakati wote linafanya kazi zake kwa kutumia kipato hicho kulingana na mipango yake, hata hivyo kanisa halitakiuka sheria na taratibu za kiserikali zinazolinda uendeshaji wa makanisa kwa uadilifu.

Kanisa la Methodist duniani ni miongoni mwa makanisa ya Kiprotestanti ambalo lilianzishwa na **JOHN WESLEY** ( **mwaka 1703-1791)** aliyekua mchungaji wa kanisa la Anglikana alitumika kama mmissionari Uingereza na Amerika.Mwaka **1862** Juni kanisa la Methodist liliingizwa Afrika mashariki katika Nchi ya Kenya na kupewa mamlaka na Uingereza kama kanisa huru.

Kanisa la Methodist Tanzania (MCT) lilianzishwa mwaka **1986,** ikiwa misheni ya kanisa la Methodist Kenya (MCK). Na mwaka **1988** likapata usajili rasmi Nchini Tanzania, Chini ya Sinodi ya Nairobi Konferensi ya Kenya

## SEHEMU YA KWANZA: UFAFANUZI

### IBARA YA 1: TAFSIRI YA MANENO

**1.** Kanuni hizi zinatoa tafsiri za mwisho wa maneno mbalimbali kwa ajili ya matumizi katika kanisa kama ifuatavyo:-

**A. ALAMA** – Ni michoro, maumbo,herufi,vitu,shughuli,picha au mavazi,Alama hizi zinaashiria au kutoa utambulisho wa imani uongozi jambo au wazo la Kikristo au kijamii kanisani alama zaweza kuwa sare,rangi kazi za sanaa iliotengeneza Maandishi,Kauli ,Tendo au Ishara za Mwili.

**B. ASKOFU** - Ni kiongozi aliyewekewa mikono atoaye huduma za kichungaji na aliye mwangalizi mkuu wa kanisa ngazi ya Sinodi kutoka miongoni mwa wachungaji wa (MCT) na kuwekewa mikono na askofu mkuu.

**C. ASKOFU MKUU** – Ni kiongozi mwangalizi wa kanisa na aliyewekewa mikono atoaye huduma za kiuchungaji na msemaji mkuu wa kanisa aliyechaguliwa na mkutano mkuu wa (MCT) kutoka miongoni mwa maaskofu wa sinodi wa (MCT)

**D. BARAZA LA MAASKOFU** – Ni kikao cha Maaskofu wa kanisa la Methodist church in Tanzania (MCT) kinachoshughulikia mambo ya imani na Theolojia pia Kumshauri Askofu mkuu katika Maono na Utume na mahusiano ndani na nje ya Nchi ya Tanzania.

**E . BODI YA WADHAMINI WA MALI ZA KANISA** – Ni wasimamizi wa mali za kanisa waliosajiliwa kwa muunganisho wa wadhamini wanaongozwa na sheria za Jamhuri ya muungano wa Tanzania ya usajili wa wadhamini sura ya **318** toleo la **2023**(**The Trustees Incoorporation Cap 318 Act RE 2002** ) na marekebisho yake yanayotumika kwa sasa.

**F. CCT:-** Christian Council of Tanzania yaani Jumuiya ya Kikristo Tanzania.

**G. SINODI:**- Ni eneo lililoidhinishwa na Baraza la Maaskofu wa (MCT) na kupitishwa na mkutano mkuu wa (MCT) inyaoundwa na saketi zaidi ya moja.

**H. MCT**:- Methodist Church in Tanzania (Kanisa la Methodist Tanzania)

**I. KONFERENSI**:-Ni chombo cha mamlaka ya mwisho ndani ya kanisa la Methodist chenye kutafsiri mafundisho ya msingi ya Imani ya Kanisa.

**J. SAKETI**:- Ni muunganiko wa makanisa zaidi ya moja

**K. KANISA**:- Jumuiya ya waumini mahali wanaokusanyika pamoja  kumwabudu Mungu.

## IBARA YA PILI: MAMLAKA YA KUTOA TAFSIRI.

Katika hali ya kawaida ya kiutendaji ndani ya kanisa endapo kuna hoja ya kutoa ufafanuzi au tafsiri ya neno ambalo halikufafanuliwa au tafsiri ya neno ambalo halikufafanuliwa au lina mkanganyiko Bodi ya idara ya sheria katiba na kanuni za MCT na Baraza la Maaskofu lililopo madarakani litakaa na kutoa ufafanuzi au tafsiri stahiki vinginvevyo mahakama ifanye wajibu wake kwa mujibu wa sheria za jamhuri ya muungano wa Tanzania

## SEHEMU YA PILI: UTAMBULISHO WA KANISA

## IBARA YA 3: JINA LA KANISA

Methodist church in Tanzania Kwa kifupi (MCT) lenye usajili **S.A NA 6945** Nchini Tanzania

## IBARA YA 4: MAKAO MAKUU

1. Makao makuu ya MCT yatakua Mwanza Tanzania  **S.L.P 221 Mwanza**
   **IBARA YA 5: NEMBO YA KANISA LA METHODIST**
   Nembo ya MCT Kama ilivyoelekezwa na kufanyiwa maboresho **Juni 2023 fungu la I uk 8.**
   **SEHEMU YA TATU: MAONO NA MALENGO NA UTUME.**
   Kwa mujibu wa katiba ya kanisa la (MCT) Fungu la III ukurasa wa 18, 19, 20, 21.iliyofanyiwa maboresho **Juni 2023**.

A. Maono ya kanisa: - Watu wote wamwabudu Mungu katika Roho na kweli na wanaishi maisha ya utoshelevu.
B. Kanuni hizi zinaelekeza uongozi wa kanisa la MCT katika ngazi zote pamoja na waumini wote kusimamia maono ya kanisa kwa vitendo ili kuhakikisha kuwa na mwelekeo mmoja.
C. Hivyo basi uongozi wa kanisa katika ngazi zote unatakiwa kutengeneza, kupitisha kutekeleza mipango na mikakati ya muda mrefu na mfupi, ikiaksi maono ya kanisa.

**IBARA YA 7: UTUME WA KANISA**

1. Vile vile utume ni kuhubiri na kufundisha injili ya Bwana wetu Yesu Kristo kwa usahihi na kumhudumia mwanadamu katika ukamilifu wake kwa msingi wa Neno la Mungu.

**IBARA YA 8: MALENGO YA KANISA**

A, Kumpenda, kumwabudu na kumtukuza Mungu

B. Kueneza injili ya Bwana wetu Yesu Kristo Nchini Tanzania, Barani Afrika na ulimwenguni mzima

C. Kuwafundisha watu Neno la Mungu na kuwabatiza wanaomwamini Yesu Kristo.

D. Kuwahudumia watu kikamilifu kiroho, kimwili na kiakili katika mazingira yao kwa kuzingatia

(i) - Huduma za kiroho

(ii)- Huduma za kiakili, kimwili katika mazingira yao

E. Kufunga Ndoa za wakristo walio wafuasi wa MCT na wenzi wao ambao ni wafuasi wa makanisa mengine wenye imani sawa na MCT wasio na lawama kanisani na kuwabariki watoto wao.
F. Kuendesha ibada za mazishi kwa msingi ya Biblila na Taratibu za (MCT)
G. Kuwashirikisha wakristo wote katika kazi za kanisa na Taifa, Kiroho na kimwili na kiakili.

H. Wamethodist wa Tanzania ni sehemu ya wamethodist ulimwenguni wanaopaswa kuuthanmini na kuenzi mafundisho na kutanabaisha kuwa:
   i) Kuamini mafundisho ya Biblia kuwa msingi wa maisha ya mkristo
   ii) Ujenzi wa Amani
   iii) Kusimamia Umoja
   iv) Kuitazana jamii kama kitovu cha maisha
   v) Msimamo thabiti juu ya ukweli.

I. Inapowezekana vingozi na waumini wa MCT wataungana na ndugu katika Fungamano la wamethodist ulimwenguni kwa malengo ya kujifunza menejimenti bora ya makanisa kubadilishana uzoefu na stadi ya jamii na uchumi endelevu na ushuhuda.

## IBARA YA 9: IMANI YA KANISA

FUNGU LA II LA KATIBA YA MCT.Toleo la katiba ilioyofanyiwa marekebisho juni 2023 ukurasa **10,11,12,13,14,15,16,** na **17** inaeleza juu ya imani ya MCT

Methodist church in Tanzania inaamini kwamba :-

1. Mungu ni mmoja katika utatu mtakatifu(**Mathayo 28:19**)
   A. Mungu Baba
   B. Mungu Mwana
   C. Mungu Roho Mtakatifu
2. Mungu ni muumba na mtawala wa vitu vyote duniani na mbinguni,Mungu aliwaumba mwanamme na mwanamke kwa mfano wake akawapa mamlaka ya kutawala viumbe vyote vya duniani (**Mwanzo 1:1**) na( **Mwanzo 1:26-28**)
3. Uungu na ubinadamu wa Mungu mwana ambaye ndiye BWANA YESU.
4. Waumini wa MCT wanaamini kwamba Biblia Takatifu (Maandiko Matakatifu) ina jumla ya **vitabu 66**.Biblia ina Agano la kale (**vitabu 39**) na Agano jipya **vitabu 27** waumini wa MCT wanaamini kuwa Biblia ni maandiko yasiyo na makosa na hivyo Biblia ndiyo yenye mamlaka ya mwisho juu ya imani ya waumini .Kanuni hizi zinaelekeza kuwa

mambo yote ya kiroho na namna ya kuendesha kanisa yatazingatia tafsiri sahihi ya Biblia.

5. Waumini wa MCT wanaamini mafundisho ya Agano Jipya juu ya kiapo na uaminifu ili tutimize ahadi kama vile: Ndoa, Ubatizo, Uongozi na nadhiri zetu kwa kumtegemea Mungu ndiyo kwetu iwe ndiyo na siyo iwe siyo.
6. Kanuni hizi zinatambua utaratibu uliopo baina ya kiapo cha kutaja jina la Mungu bure na vitu vyote alivyoviumba (kujiapiza) kwa manufaa binafsi dhidi ya kiapo cha kuweka nadhiri kwa mujibu wa sheria kanuni na taratibu zianzoongoza katika mazingira husika. (**Mathayo 6:14-15**)
7. Waumini wa MCT wanaamini mafundisho ya Agano jipya juu ya kudumu katika Amani Upendo,Msamnaha na kutolipiza kisasi (**Rumi 12:18,1 Korr.13:1-3,Mathayo 6:14-15,Mathayo 5:39-44**)
8. Kanuni hizi zinazuia waumini wa MCT kuanzisha .Kuchochea au kufadhili vita machafuko na ugomvi katika kanisa, jamii na Taifa.
9. Kanuni hizi zinawaelekeza waumini wa MCT juu ya wajibu wao katika kuleta upatanisho, Msamaha na kujenga amani katika kanisa, Jamii, Taifa na Duniani kwa ujumla.
10. **Imani ya Mitume**.
    A. Waumini wa MCT wanakiri Imani ya Mitume inayotuunganisha sisi na waumini wengine wakristo Duniani kwamba ‘’Namwamini Mungu Baba Mwenyezi,Muumba wa mbingu na Nchi,na Yesu mwana wake wa pekee,Bwana wetu; aliyechukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu akazaliwa ;akashuka mahali pa wafu; Siku ya tatu akafufuka ;Akapaa Mbinguni;Ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyezi;Kutoka huko atakuja kuwahukumu walio hai na walio wafu;Namwamini Roho Mtakatifu;Knisa Takatifu lililo Moja ;Ushirika wa watakatifu;Ondoleo la dhambi;Kiyama ya mwili,na uzima wa milele,Amina.’’

B. Kanuni hizi zinasisitiza kwamba kila inapofanyika ibada kwa mujibu wa taratibu za ibada za MCT inayotumika katika kanisa la MCT Ukiri huu Imani lazima Isemwe.

**11.Msalaba wa Ukombozi**

A. Waumini wa MCT wanaamini kuwa msalaba wa Yesu Kristo ni alama ya Ukombozi wa Mwanadamu kutokana na kifo na kufufuka kwake kwa njia ya msalaba,Yesu kristo akaleta,ondoleo la dhambi na kutupatanisha na Mungu mwenyezi kwa msalaba tunaona upendo wa Mungu,Tumaini la wokovu wetu.Na kwa msalaba kanisa la watakatifu lilioanzishwa lenye ahadi ya uzima wa milele.(**Efeo 2:16:Kol 1:20-22,Korr 1:1:17-18**)

B. Kanuni hizi zinatambua matumizi halali ya msalaba wa Yesu Kristo kama ilivyopitishwa na mkutano mkuu wa Konferensi kwa mujibu wa Biblia na katiba ya (MCT)

**12.Kurudi kwa Yesu Mara ya Pili.**

A. Waumini wa MCT wanaamini na kukiri juu ya kurudi kwa Yesu Kristo kwa mara yya pili kama alivyoahidi kabla ya kupaa kwake kwenda mbinguni .Na kurudi kwake atalichukua kanisa la waaminifu na kuishi nalo milele huko mbunguni.(**Yoh 14:1-3,** 1**Thesa 4:16-17**)

B. Kanuni hizi zinasisitiza Imani hii kuchukuliwa kwa umuhimu wake katika mafundisho ya kanisa ili kuandaa kanisa kwa ajili ya maisha ya utukufu ujao baada ya maisha ya hapa Duniani.

**13.Ubatizo**

A. Waumini wa MCT wanaamini na kukiri juu ya ubatizo wa maji mengi au machache lakini pia waumini wa MCT wanaamini kuwa ubatizo ni ushuhuda wa nje wa kumpokea Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yao.(**Mt 3:11,Mdo 2:37-41**)

B. Katika mazingira ya kawaida kanuni hizi zinaelekeza kuwa watakaoabatizwa watakuwa wamefuzu mafundisho ya kateksimo na wamekiri juu ya Imani ya MCT.

C. Ktaika mazingira yasiyo ya kawaida kanuni hizi zinatoa nafasi ya mtu kubatizwa pasipo kutimiza matakwa yaliyowekwa

D. Utaratibu wa kufuatwa wakati wa ubatizo ni ule uliolekezwa katika kitabu cha utaratibu wa ibada cha Methodist church in Tanzania. (MCT)
E. Kanuni hizi zinazingatia utekelezaji wa katiba ya MCT maboresho ya Juni 2023.FUNGU LA IX UK 138 na kuwa viongozi wote ndani ya MCT wanatakiwa kuwa na Ndoa ya Kikristo.Na kila mwenye Ndoa apeleke Nakala ya cheti kwa Mchungaji wake wa saketi
F. Kwa kuwa katiba ya MCT haipingani na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .Kanuni hizi zinaagiza kuwa Ndoa zifungishwe na Askofu au Mchunagaji mwenye Leseni hai na si vinginevyo.Na kwamaba waumini na viongozi wa kanisa wataheshimu maamzi ya mahakama Juu ya ukomo wa Ndoa.
G. Kanuni hizi zinaelekezwa kuwa endapo itabainika na mamlaka ya kinidhamu katika ngazi husika ya MCT kuwa mwenza wa muumini/Kiongozi ndiye amekengeuka na kutodumisha kutoheshimu nadhiri ya Ndoa yao na au kusababisha ukomo wa Ndoa kisheria pasipo muumini/kiongozi tajwa kusababisha muumini/kiongozi hatachukuliwa hatua zote za kinidhamu na hiyo ataendelea kuwa na haki na hadhi yake ya muumini/kiongozi na kama Ndoa yao imefika ukomo kwa kisheria za Nchi muumini/kiongozi husika apewe ushauri nasaha na atakuwa huru kuoa /kuolewa katika Ndoa takatifu mbele ya madhabahu.

16. **Kuweka Watoto Wakfu**

A. Waumini wa MCT wanaamini kuwa watoto hawawezi kuamini na kumpokea Yesu Kristo kama Bwana na mwokozi wa maisha yao.Kwa maana Bwana wetu Yesu Kristo aliwabariki watoto, MCT Iinaruhusu kuwaweka wakfu watoto ili wakue katika kicho cha Kristo mpaka hapo watakapofikia hatua ya kukata shauri wenyewe(**Mk 10:13-16,Mt 19:13-15,Lk 18:15-17**)

B. Kanuinin hizi zinaelekeza wazazi/mzazi/mlezi kutoa ahadi mbele ya madhabahu mbele za Mungu na waumini kumlea mtoto katika kicho cha Kristo.

C. Kanuni hizi zinaelekeza kuwa utaratibu wa kuwaweka watoto wakfu kwa Bwana uzingatie maelekezo yaliyotolewa mwongozo na Taratibu za ibada za MCT.

D. Kanuni hizi zinaweka zuio la kumbagua mtoto yeyote na kunyimwa haki ya kuwekwa wakfu kwa Bwana kwa sababu zozote zile.

## SEHEMU YA 10: UFUASI NA USHIRIKA

### IBARA YA 10: UFUASI NA USHIRIKA

Methodist church in Tanzania – (MCT) inatambua waumini na washirika kama ifuatavyo:

1. Waumini wa kanisa la MCT hawa ni wakristo ambao ndio wenye mali za kanisa waumini nguzo za kanisa kupokelewa na kutambulishwa na MCT
2. Washiriki hawa hujumuisha watoto,vijana ,watu wazima wake kwa waume ambao ni marafiki wageni,wanafunzi wa kateksimo,waumini waliotengwa wanaohudhuria ibada na wengine wanaohudhuria ibada na kushiriki shughuli mbalimbali za MCT.
3. Kanuni hizi zinatanabainisha haki na wajibu wa waumini na mshiriki wa MCT.

### A. HAKI ZA MUUMINI

i) Atashiriki ibada ya Neno la Mungu kwa mujibu wa mwongozo wa Taratibu za ibada za MCT unaotumika

ii) Atashirirki mikutano mabalimbali inayomhusu kwa mujibu wa katiba ya MCT

iii) Atachagua au atachaguliwa katika nafasi za uongozi kwa mujibu wa katiba ya MCT

iv) Atapata taarifa mbalimbali za maendeleo ya kanisa kwa kufuata taratibu zilizowekwa

v) Atashiriki meza ya Bwana (ushirika mtakatifu) kwa mujibu wa mwongozo wa taratibu za ibada ya MCT

vi) Kwa kufuata mwongozo wa utaratibu wa ibada wa MCT unaotumika muumini au kiongozi atamleta mwanaye Au wanawe

kwa mchungaji kwa ajili ya kuwaweka wakfu au kupata mafunzo ya kateksimo au kupokelewa kanisani

vii) Kwa kufuata mwongozo wa utaratibu wa ibada wa MCT na sheria za Nchi zinazotumika atafunga Ndoa takatifu

viii) Atatunzwa na kulelewa kiroho kwa mujibu wa imani ya MCT

ix) Katika tuhuma yeyote inayomkabili atapewa Fursa ya kusikilizwa na pia kukata rufaa inapobidi

x) Akiona au akigundua makosa au ukiukwaji unaotendeka katika ngazi yake ,atapewa fursa ya kutoa taarifa au malalamiko katika ngazi husika kwa mujibu wa taratibu za kinidhamu na usuluhishi wa migogoro

xi) Kupitia Baraza la Bodi ya wadhamini wasajiliwa; waumini wa MCT wanamiliki fedha na mali za MCT na wana haki ya kupanga matumizi yake kutekeleza madhumini ya MCT kwa mujibu wa katiba ya MCT.

xii) Haki nyinginezo kama zitakavyoamriwa na mikutano husika ya MCT

## B. WAJIBU WA MUUMINI

i) Atahudhuria na kushiriki kikamilifu ibada za MCT ngazi zote,

ii) Atatoa zaka sadaka,matoleo ya ahadi,shukrani na michango mbalimbali inayokubalika katika ngazi husika

iii) Atajitolea kwa nguvu,mali zake zote na akili kwa kuwatunza watumishi wa kanisa

iv) Atajitolea kwa nguvu,Akili na mali zake kuchangia maendeleo ya kanisa

v) Atahudhuria na kushiriki kikamilifu mikutano inayomhusu kwa mujibu wa katiba ya MCT

vi) Atajenga na kutunza umoja na Amani ndani na nje ya kanisa

vii) Atalinda fedha na mali za kanisa

viii) Atachangia mawazo yenye kuleta ufanisi na atatoa taarifa za kweli kwa ngazi husika.

ix) Ataheshimu,atatetea na kulinda katiba ya MCT na kanuni zake

x) Atakuwa na wajibu mwingine kama itakavyoamriwa na mikutano husika ya MCT

## C. KUMWANDIKA MUUMINI WA MCT

i). Muumini mpya aliyebatizwa

1. Mwanafunzi wa kateksimo aliyebatizwa kwa mujibu wa taratibu za ibada za MCT atatambulishwa na mchungaji husika atamkumbusha juu ya haki na wajibu wake.

2. Aliyebatizwa atapewa cheti cha ubatizo na mchungaji mhusika

3. Katibu wa makanisa la mahali atamworodhesha muumini mpya katika daftari la waumini ambalo ni sehemu ya taarifa za MCT/saketi na kanisa la mahali

ii. Muumini mpya atakayehamia MCT kutoka dhehebu jingine la kikristo aliyebatizwa ataomba kujiunga na MCT .Atawajibika kuleta utambulisho wa ukristo wake kutoka katika uongozi wa kanisa analotoka

## D. UKOMO WA MUUMINI WA MCT

i) MCT inakubali kuwa muumini/Mkristo wa MCT anaweza kukoma kutokana na sababu mbalimbali na hivyo muumini huyo atahesabika kutokuwa na haki na wajibu wa muumini.Sababu za ukomo wa muumini ni kama ifuatacvyo:-

1. Kuacha Imani ya MCT na kusimamishwa kwa taratibu za kanisa
2. Kujitoa kwa hiari yake mwenyewe au kuhama kanisa .kujitoa au kuhama kutohalalishwa kwa muumini kuandika barua kwa mchungaji wa saketi.Endapo muumini hataandika barua Baraza la saketi litajadili shauri hilo na kutoa uamuzi.

E. Kanuni za kufuata kumrejesha muumini aliyesimamishwa endapo atajibu, atajutia makosa yake na kutubu.

1. Atatakiwa ahudhurie ibada za MCT kama mshiriki

2. Ataandika na kuwasilisha barua ya ombi  la kurejea kwa mchungaji wa saketi
3. Baraza la saketi husika litajadili ombi hilo na akikubaliwa ataandikiwa barua na kurejeshwa huku akikumbushwa haki na wajibu wake kama muumini wa MCT.Vinginevyo atajulishwa sababu za kutokubaliwa.
4. Fursa ya kuomba kwa mara nyingine kurejea kanisani itakuwa kwa anayehitajika.

## SEHEMU YA 5: UONGOZI

### IBARA YA 11: VIONGOZI WA KANISA

*A.* Kanisa la MCT lina viongozi wanatambulika katika ngazi mbali mbali kuanzia ngazi ya kanisa la mahali,saketi sinodi hadi konferensi (Rejea Fungu la V la katiba ya MCT iliyofanyiwa maboresho Juni 2023 viongozi hao ni kama ifuatavyo*:*-

#### i). Kanisa la mahali

1. Mchungaji wa Kanisa
2. Mwinjilisti  wa kanisa
3. Mzee wa Kanisa
4. Katibu wa kanisa
5. Mtunza hazina wa kanisa
6. Shemasi wa kanisa

#### ii). Saketi

1. Mchungaji Kiongozi
2. Mchungaji
3. Katibu wa Saketi
4. Mtunza hazina wa saketi
5. Mwinjilisti
6.

### iii). Sinodi

1. Askofu
2. Katibu
3. Mtunza Hazina wa Sinodi

### iv). Konferensi

1. Askofu Mkuu
2. Katibu Mkuu
3. Mtunza Hazina

B. Kanuni hizi zinaweka utaratibu wa viongozi kuwatayarisha na kuwaingiza kazi kusimamia utendaji wao,kuwaelimisha na kuendeleza maslahi yao na motisha ushirikishwaji na utaratibu,uwajibikaji kusimamia madaraka,mahusiano kazini,Utatuzi wa migogoro na ukomo wa utumishi wao.Ufuatao ni ufafanuzi katika kutekeleza kifungu hiki cha B;

**1. Kuwapata Viongozi**

**i).** Viongozi wote wa kuchaguliwa kuteuliwa au kuajiriwa wapatikane kwa kufuata UTARATIBU na SIFA zilizotajwa kwenye katiba Rejea FUNGIU LA V. Toleo la Juni 2023 katiba ya MCT

**II).** Viongozi watakaowekewa mikono ni maaskofu na wachungaji mara baada ya kuchaguliwa na kusaini hati za viapo vya uaminifu wa utumishi

**iii).** Makatibu kuanzia ngazi ya kanisa la mahali, saketi, sinodi na konferensi wa MCT wataanzisha kazi data za waumini na viongozi wote kila mtumishi/kiongozi atakuwa na faili lake lenye taarifa muhimu watatetuliwa viongozi watakaosimamia uchaguzi M/kiti na katibu na wasidizi wao kisha majina yatapendekezwa kupigiwa kura watasimamia uchaguzi na watatoa matokeo na kuandika taarifa ya uchaguzi kwa ajili ya kumbukumbu za kanisa na kukabidhi kwa mwenye kiti wa kiakao ngazi husika.

**v).** Kabla ya kupiga kura ni vema yakazingatiwa mambo yafuatayo:

1. Sifa stahiki za kazi husika

2. Mamalaka ya uwajibikaji na mipaka ya kazi husika
3. Eneo la kazi husika
4. Utaratibu wa mapendekezo hadi uchaguzi
5. Taratibu za upigaji Kura

**vi**). Kanuni hizi zinaagiza kuwa msimamizi wa uchaguzi atasimamia uchaguzi na kutangaza matokeo ya uchaguzi na ya mkutano husika wa uchaguzi siku hiyo hiyo.

**vii).** Kanuni hizi zinaagiza kuwa wakati wa uchaguzi wajumbe halali watapiga kura za siri na msimamizi wa uchaguzi atatangaza matokeo

**viii)**. Kanuni hizi zinaelekeza kuwa ukiukwaji wowote wa taratibu za kuwapata viongozi na wajumbe ni kosa litakalosababisha mhusika kuadhibiwa.

**2. Kuwatayarisha na kuwaingiza kazini**

**i)**. Utaratibu wa kuwatayarisha viongozi wa kanisa utakuwa ni wa lazima kwa mujibu wa katiba ya MCT na kanuni zake.

**ii)**. Viongozi wataelezwa na mamlaka ya kanisa kwenye ngazi husika na kupewa maelezo ya kina juu ya dira ya kanisa,wajibu wao,majukumu yao,mipaka yao,uwajibikaji na mazingira ya kazi yao kupitia semina elekezi  kwa kuwashirikisha wataalamu mbalimbali wa ndani na nje ya ya MCT

**iii)**. Kiongozi aliyechaguliwa/kuchaguliwa/kuteuliwa ataingizwa kazini na kutambulishwa na mamalaka ya ngazi husika mara moja kwa mujibui wa katiba ya MCT

**IV**). Kiongozi au mjumbe yeyote ataingizwa kazini kwa kuweka ahadi,za utiifu,uaminifu na uwajibikaji.

**v)**. Kila mara patokeapo mabadiliko ya uongozi kutakuwepo na, makabidhiano ya ofisi, fedha, mali, nyaraka na taarifa mabalimbali kwa maandishi.Nakala za makabidhiano zipelekwe kwa ngazi ya juu.

3. **Utekelezaji wa majukumu na mipaka ya kazi**

A. Kila kiongozi atawajibika kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia mgawanyo wa kazi na majukumu mipaka na muundo wa kanisa na taasisi zake kwa mujibu wa katiba ya MCT.

B. Kila kiongozi aelekezwe atawajibijika kwa nani na ni akina nani wanawajibika kwake.Hivyo, kanuni hizi zinazuia kiongozi yeyeote kuingilia na kuvamia madaraka na mamlaka yasiyo yake.

C. Kanuni hizi zinaelekeza viongozi kuepuka utendaji kwa maslahi binafsi.Hairuhusiwi kwa kituo au asasi kwa ngazi zote za kanisa,Kanisa la mahali,saketi sinodi na Konferensi kuongozwa na viongozi wa familia moja,kuepuka ubinafsi na migongano ya kimaslahi kwenye utendaji na mfumo wa uwajibikaji.

**IBARA YA 12: UUTUMISHI NDANI YA KANISA**

4: (A). **Watumishi wa kiroho ndani ya kanisa**

1). Mwinjilisti atawajibika kwa mchungaji

2). Mzee wa kanisa atawajibika kwa mwinjilisti

3). Shemasi atawajibika kwa mzee wa kanisa

4). Mchungaji atawajibika kwa mchungaji kiongozi

5). Mchungaji kiongozi atawajibika kwa Askofu

6). Askofu atawajibika kwa Askofu mkuu

7) Askofu mkuu atawajibika kwa mkutano mkuu wa konfaransa

(B) **Watumishi Walezi**

1. Katibu atawajibika kwa kiongozi mkuu mwenyekiti wa ngazi yake husika

2. Mtunza hazina atawajibika kwa katibu wa ngazi yake husika

3. Mwenyekiti wa Bodi ya idara atawajibika kwa katibu wa ngazi yake husika.

4. Mwenye kiti wa Bodi ya utawala ya taasisi/mradi program-atawajibika kwa mwenye kiti wa bodi ya idara husika.

5. Mkuu wa idara atawajibika ka katibu ngazi yake husika.

6. Mwenyekeiti wa jumuiya atawajibika kwa katibu wa ngazi yake husika

7. Katibu wa jumuiya atawajibika kwa mwenyekiti wa jumuiya yake kwa ngazi husika

5. **Kusimamia utendaji wao**

i). Kanuni hizi zinaagizwa kutengenezwa kwa mpango kazi katika kila ngazi za kanisa na kutumika ipasavyo

ii) Utendaji kazi wa kila kiongozi utatathiminiwa (kupimwa)na msimamizi wake kwa vigezo vya mpango mkakati/mpango kazi na viashiria vya ufanisi wa kazini.Tathimini ya utendaji kazi utafanywa kwa kila robo mwaka au nusu mwaka na baada ya mwaka.

iii). Tathimini ya utendaji kazi itatolewa taarifa kwa maandishi na makal;a zitatolewa kwa mhusika na pia ofisi husika.

iv). Tathimini ya utendaji kazi itumike kufanya maboresho ya utendaji na Kwa ajili ya motisha.

**IBARA YA 13: HAKI NA TARATIBU ZA UTUMISHI**

Kanuni hizi zinafafanua mambo ya haki kazi ukomo wa kazi na taratibu mbalimbali za kiutumishi zinazopaswa kufuatwa kwa viongozi na watumishi wa MCT

B. Anayeajiriwa/anayechaguliwa anayeteuliwa ndani ya MCT na katika idara, jumuiya, Taasisi, miradi na program za MCT atapewa mkataba wa ajira wenye

Saini maelezo ya kazi (Job descriptions) na katibu wa ngazi husika.

C. Anayeajiriwa /anayeteuliwa/anayechaguliwa na MCT na katika idara,jumuiya,taasisi miradi na program za MCT anapaswa kujaza na kuweka saini fomu maalum inayotaja masharti ya utumishi na maadili ya jumla ya kanisa akikiri kwamba atayafuata kwa mujibu wa katiba ya MCT

D. Kanisa katika ngazi zote kupitia ofisi, Baraza la maaskofu au kamati tendaji au mwinjilisti na kumpeleka katika kituo kingine ndani au nje ya sinodi ama sakleti kulingana na uhitaji na sababu za msingi kwa idhini ya kamati tendaji na alipo mtumishi huyo.

E. Maaskofu,wachungaji,wainjilisti/watendaji wa kanisa ,idara,taasisi miradi na program za MCT .Ni watumishi wa kanisa kupitia kamati kuu za ngazi husika,hivyo watalipwa stahiki na maslahi yao inavyoelekezwa katika kanuni hizi.

i). Askofu mkuu-atalipwa ujira na stahiki zake kutoka ofisi ya konferensi.

ii). Askofu atalipwa ujira na stahiki zake kutoka sinodi anayoongoza

iii. Mchungaji kiongozi na wachungaji wa kawaida watalipwa ujira na stahiki zao kutoka katika saketi wanayoiongoza

iv). Katibu wa MCT atalipwa ujira na stahiki zake kutoka ofisi ya MCT

v). Mtunza hazina wa MCT atalipwa ujira na stahiki zake kutoka ofisi ya MCT

vi. Katibu wa sinodi atalipwa ujira wake na stahiki zake kutoka ofisi ya sinodi

vii). Mtunza hazina wa Sinodi atalipwa ujira na stahiki zake kutoka ofisi ya sinodi

viii). Watendaji wa idara ,jumuiya na taasisi miradi na program za MCT .walioajiriwa na walioteuliwa watalipwa ujira na stahiki zao kwa mujibu wa mikataba yao.

F. Umri wa kustaafu kwa watumishi wa kanisa wa kuchaguliwa ni miaka sitini na tano tu!. (65)Umri wa kustaafu kwa watumishi wa kuajiriwa(wafanya kazi) wa kanisa ufuate utaratibu wa ajira za serikali zitakazo kuwepo kwa muda huo.

G. Endapo kanisa litaona haja ya kuendelea kumtumia mtumishi/watumishi aliyestaafu, kamati tendaji ya ngazi husika au Bodi ya utawala inayohusika na mtumishi huyo kulingana na haja iliyopo itamwomba akikubali ataingia mkataba wa ajira.
H. Katika uongozi wa kuchaguliwa au kuteuliwa izingatiwe kuwa mgombea hatakuwa na miaka zaidi ya umri wa kustaafu kabla ya kumaliza kipindi chake cha uongozi.
I. MCT. Idara ,taasisi,jumuiya au program za MCT zaweza kuajiri,kuteua kuchagua watumishi wenye sifa ambao si raia wa Tanzania na kuwapa majukumu mbalimbali kwa mkataba ya kazi husika.Kanuni hizi zinaagiza kuwa katibu mkuu wa MCT ahakikishe watumishi wasio raia wana vibali vya kazi na ukazi husika kabla ya kuanza kazi kwa mujibu wa sheria na kanuni huisika za jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
J. Wamisionari wote wanaingia Nchini kufanya kazi na MCT watajaza fomu za maombi kwenye ofisi ya Askofu na ofisisi ya MCT itasimamia mikataba yao ya kazi baada ya kukubaliwa
K. Ofisi ya MCT ndiyo yenye mamlaka ya kutuma wamisionari kwenye saketi au sinodi au MCT kulingana na huduma ya Mmisionari huyo.
L. Taarifa zote za utendaji kazi za wamisionari zitatumwa kwa katibu wa MCT na katibu atazipeleka kamati tendaji kupima utenda kazi wao.

## IBARA YA 14: BODI YA WADHAMINI ILIYOSAJILIWA MCT

A. Kanuni hizi zinatambua kuwepo kwa Bodi ya wadhamini kama inavyoelekezwa katika FUNGU la VI la katiba ya MCT Toleo la Juni 2023 ukurasa wa 84,85,86 na 87.Lakini pia katika sheria ya wadhamini sura ya 318 RE Toleo 2023 The Trustees Incoorporation Act Cap 318 RE 2002 na marekebisho Yake.
B. Bodi hii itawajibika Kwa mkutano mkuu wa MCT.Bodi ya wadhamini itakutana mara mbili Kwa mwaka.
C. Uchaguzi wa bodi ya wadhamini waliosajiliwa utafanya na Mkutano mkuu wa MCT kila baada ya miaka mitano (5) ya kipindi cha kuwa madarakani.M/kiti wa Bodi ya wadhamini atachaguliwa na wajumbe wa Bodi waliochaguliwa na mkutano mkuu wa MCT
D. Wajumbe wa Bodi ya wadhamini watakaochaguliwa na mkutano mkuu wa MCT ni hawa wafuatao:-

1. Wachungaji watatu (3) ( wenye elimu na uwezo wa kutosha kuelewa mambo mbali mbali)
2. Wakristo wane (4) wanaume wawili na wanawake 2 wenye elimu na kujua mambo mbalimbali
3. Na watachaguliwa baada ya miaka mitano (5)

   A. Sifa za wajumbe wa Bodi ya wadhamini

      i) Awe mkristo-Muumini wa MCT mwenye nia njema
      ii) Awe raia mwema wa Tanzania
      iii) Awe ni mtu mwenye heshima,mwaminifu na ushuhuda uliotukuka
      iv) Awe na afya njema ya kumudu majukukmu yake
      v) Awew na uwezo wa kjutumia lugha zote mbili ya Kiingereza na Kiswahili
      vi) Asiwe muajiriwa wa serikali au MCT
      vii) Asiwe aliyehukumiwa mahakamani kwa makosa ya jinai ya udanganyifu au ubadhilifu
      viii) Asiwe mtu ambaye ametangaziwa kufilisiwa/kufilisika kwa asasi anayomiliki/ongoza .

   B. Majukumu ya Bodi ya wadhamini

      i) Bodi hii itatekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na katibu mkuu wa MCT na kutoa taarifa zake kwenye mkutano mkuu kupitia kamati tendaji ya MCT wajumbe wa bodi ya wadhamini watakuwa wajumbe halali wa kamati tendaji ya MCT na mkutano mkuu wa MCT.

   Majukumu ya Bodi ya wadhamini ni?

   1. Kuhakikisha mali zote za MCT zinazohamishika na zisizohamishika kama vile:Viwanja,Nyumba,Magari,Mitambo,Vyombo vya Teknolojia ya mawasilioano,Mihuri,Mikataba,Mali ghafi,Fedha,,Vitabu vya kanisa na kutunzwa vyema kwa mujibu wa sheria za Nchi
   2. Kupendekeza kwa kamati tendaji na mkutano mkuu wa MCT kuhusu upatikanaji wa mali za kanaisa iliosajiliwa na serikali

3. Kupokea na kutathimini taarifa ya mkaguzi wa nje ( external Auditor) wa mali na fedha za kanisa na mthaminishaji) ( Fixed Asset valuer) wa mali za kanisa aliyesajiliwa na serikali
4. Kutoa idhini ya maandishi kwa MCT sinodi ,idara Taasisi na miradi husika kwa mujibu wa sera na kanauni zitumikazo .Idhini yao itakuwa ni kwa mali moja moja yenye thamani isiyopungua Tshs.10,000,000/=
5. Mali zingine zilizo chini ya sinodi na MCT zenye thamani ya chini ya Tshs. 10,000,000/= zitatolewa idhini na kamati tendaji.Zile zilizo chini ya taasisi na miradi zitatolewa idhini na Bodi za utawala wa idara ,taasisi na miradi husika.
6. Kusuluhisha migogoro mikubwa ndani ya kanisa ambayo imeshindikana katika ngazi zote za kanisa MCT ni chombo cha mwisho cha rufaa cha mwisho kinacho shughulikia migogoro ndani ya MCT
7. Kuteua mfilisi aliyesajiliwa na serikali endapo atahitajika wakati wa kuvunjika kwa kanisa taasisi au miradi/mpango wa kanisa
8. Kupitia katibu mkuu wa MCT kutafuata kibali cha kumiliki ardhi toka kwa kabidhi wasihi mkuu
9. Inapobidi (Hatua za mwisho)kumshtaki mtu/Asasi mahakamani kwa niaba ya kanisa
10. Kupitia katibu mkuu wa MCT kuwasilisha marejesho ya mwaka (yearly returns) kwa kabidhi wasihi mkuu
11. Kupitia kwa katibu mkuu wa MCTkuwasilisha taarifa mbali mbali za majukumu kama vile mabadiliko yoyote ndani ya kanisa kwa mfano,wadhamini ,Viongozi ,Anuani,Makao makuu ya MCT kwa kabidhi wasihi mkuu ndani ya mwezi moja tangu mabadiliko hayo yafanyike .Pia mwenyekiti wa Bodi atawasilisha kwenye vikao vya kamati tendaji na mkutanop mkuu wa MCT

C. Ukomo wa Bodi ya wadhamini
   1. Atakapougua ugonjwa wa akili

2. Atakapougua ugonjwa utakaomfanya asiweze kuona ,kusikia,kutembea na kuzungumza
3. Atakapobainika kushindwa kuwa mwaminifu kwa mali za MCT
4. Atakapo fariki
5. Atakapojiuzulu
6. Asipo chaguliwa tena

## SEHEMU YA SITA: UTARATIBU WA UCHAGUZI NA AJIRA

### IBARA YA 15: ASKOFU MKUU

Katika kanuni hizi zinatambua kuwa kwa mujibu wa katiba ya MCT Fungu la VI la katiba ya MCT (iliyofanyiwa maboresho toleo la Juni 2023) Utaratibu wa uchaguzi utakuwa kama ifuatavyo

1. Askofu Mkuu ( Presiding Bishop)
   A. Askofu mkuu ni kiongozi mwangalizi wa kanisa la MCT konfaransa na kanisa
   B. Atahudumu katika nafasi hiyo kwa wa miaka 5 na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi hicho mara moja na baada ya hapo haruhusiwi kugombea nafasi hiyo atakuwa Askofu mstaafu
   C. Askofu mkuu atachaguliwa miongoni mwa maaskofu wa sinodi na maaskofu wa sinodi ambao hawajawahi kushika wadhifa huo.

**KAZI ZA ASKOFU MKUU**

1. Kuitisha faragha ya maaskofu wa MCT mara mbili kwa mwaka kumwomba alijenge ,kuimarisha na kudumisha amani katika kanisa kwa kuleta mambo yote mbele yake kwa maombi
2. Kuwa mwenmyekiti wa mabaraza yafuatayo:-
   i) Mkutano mkuu wa konferensi
   ii) Baraza la Maaskofu
   iii) Mkutano Mkuu wa kamati tendaji
3. Kusimamia mkutano wa uamsho wa kanisa zima utakaofanyika kila sinodi kila mwaka kusudi la:

A. Kuleta uamsho kwa watu wa Mungu kwa kumwabudu na kumwomba Mungu na kuhubiri na kufundisha Neno la Mungu
B. Kufanya tathimini ya maendeleo ya kanisa zima

4. Kuwawekea maaskofu mikono wateule wa MCT kwa kushirikiana na maaskofu wa MCT pamoja na maaskofu wa makanisa ya kiinjili yanayoshirikiana na MCT na kushirikiana katika mialiko kama hiyo katika makanisa yao.
5. Kuwasimika kazini maaskofu wa MCT kwa kushirikiana na maaskofu wengine wa MCT
6. Kuwa msimamizi na mlinzi wa katiba ya MCT
7. Kuzitemebelea sinodi zote za MCT ili kufahamu kazi za kanisa zima zinavyoendeshwa na jinsi kanisa ilivyokuwa na kuimarisha na kushauriana na maaskofu wa sinodi katika maswala mbali mbali ya maendeleo ya sinodi ndani na nje ya Tanzania.
8. Kupanga Mikutano ya Konferensi ya kawaida na dharura na mikutano ya Baraza la maaskofu kujenga na kuimarisha uhusiano na makanisa mbali mbali na makundi mengine yenye imani tofauti na MCT ndani na nje ya Tanzania
9. Kusimamia kwa karibu na kuchukua hatua zinazostahili kuhakikisha migogoro inayojitokeza inatatuliwa katika muda mfupi kwa mujibu wa katiba ya MCT Fungu la X Toleo la Juni 2023.
10. Kusimamia shughuli za maendeleo ya kanisa la MCT
11. Kuwawekea mikono wachungaji wateule wa MCT kwa kushirikiana na maaskofu wengine watakao kuwepo

C. Mke wa Askofu Mkuu
   i. Mke wa Askofu mkuu ndiye mwangalizi wa idara ya akina mama ngazi ya konferensi akishirikiana na mratibu wa jumuiya ya wanawake na viongozi wa wanawake kuiongoza jumuiya hiyo.
   ii. Mke wa Askofu Mkuu ndiye kiongozi mshauri wa wake wa wachungaji anayeweza kuwafundisha na

kuwaombea katika ndoa zao na malezi kwa waume zao na watoto wao.

**IBARA YA 16: ASKOFU WA SINODI**

Askofu wa sinodi ni kiongozi msimamizi wa sinodi ya MCT na atawajibika kwa konferensi ,Askofu Mkuu Baraza la Maaskofu ,Mkutano Mkuu wa Konfaransa kamati tendaji ya konfaransa.

**A. SIFA ZA ASKOFU WA SINODI**

1. Awe na umri wa kuanzia miaka 35 na kuendelea
2. Awe na Diploma ya theolojia na kuendelea aliyoipata katika chuo kinachotambulika na MCT
3. Awe na uzoefu wa kazi ya uchungaji usiyopungua miaka mitano (5) ndani ya kanisa la MCT.
4. Awe na maono ya kujenga kanisa na kusimamia kazi za kuliongoza kanisa kwa unyenyekevu na uadilifu.

**B. KAZI ZA ASKOFIU WA SINODI**

1. Kuwa kiongozi na msemaji mkuu wa sinodi kwa kutimiza yafuatayo:-
   i). Kuhubiri
   ii). Kuomba
   iii). Kutoa ushauri wa kiroho
   Iv). Kubatiza
   v). Kushirikisha meza ya Bwana
   vi). Kufanya kazi zingine za Kichungaji
2. Kuwajibika kwa kamati tendaji ya konfernesi Askofu mkuu, Baraza la maaskofu, kamati tendaji ya Sinodi.
3. Kuitisha na kuwa mwenyekiti wa mikutano ya sinodi na kamati tendaji ya sinodi
4. Kuitisha mikutano ya sinodi na dharura
5. Kuwawekea mikono wachungaji wateule kwa kushirikiana na Askofu mkuu pamoja na maaskofu wenyeji watakao kuwepo
6. Kushiriki kuwawekea mikono wachungaji wateule wa MCT
7. Kumshauri Askofu mkuu katika utekelezaji wa maono, utume, na madhumuni ya kanisa.

8. Kumshauri Askofu mkuu juu ya mahusiano ya kanisa na madhehebu mengine nje ya kanisa.
9. Kushiriki katika kutatua migogoro ya kiroho na utawala atakayopokea kutoka kwa Askofu mkuu
10. Kushiriki katika kazi zingine za Baraza la Maaskofu Kama itakavyopendekezwa na Askofu mkuu.
11. Kutembelea saketi zote katika sinodi
12. Kufuatilia utekelezaji wa uamzi wa konferensi na kamati tendaji ya sinodi.
13. Kuongoza mkutano mkuu wa MCT utakaofanyika katika sinodi.
14. Kusimamia nidhamu ya wachungaji na wainjilisti wote katika sinodi ikiwa ni pamoja na kusimamisha mchungaji au mtumishi anayetuhumiwa kukiuka katiba kanuni na taratibu za kiutumishi na kuitisha mapema kamati tendaji kabla ya kuripoti kwa Askofu mkuu kwa maamuzi ya mwisho
15. Kuitisha faragha ya wachungaji katika sinodi
16. Kuongoza ibada ya kumzika mchungaji
17. Kuongoza ibaada ya mchungaji aliyestaafu kazi ya uchungaji

C. Askofu Ataacha kuwa Askofu kama:

i). Atajiuzulu kwa hiari kwa kutoa taarifa ya miezi mitatu

ii). Atatakiwa kujiuzulu kwa taarifa ya Daktari

iii). Atavuliwa Uaskofu kwa kuthibitika katika mkutano wa kamati tendaji ya MCT kwa kufanya tendo la dhambi

1. Kuuwa mtu kwa kukusudia
2. Wizi wa aina yeyote
3. Uzinzi na Uasherati
4. Unyanyasaji wa kijinsia
5. Ulevi wa aina yeyote( pombe,mihadarati na dawa za kulevya)
6. Kutumia vibaya misaada inayotolewa na wafadhili
7. Kujihusisha na jambo lolote ambalo kulingana na sheria za Tanzania ni kosa la jinai au uhujumu uchumi.

Iv, Atapatikana na hatia katika mahakama na akahukumiwa kifungo

v. Ataendelea kuishi maisha yaliyo kinyume na Neno la Mungu licha ya kuonywa na kushauriwa kujirekebisha

Vi.Ataipotosha au kusimamia ukweli wa Neno la Mungu

vii. Atashindwa kusimamia au ataipotosha kwa makusudi katiba ya MCT.

viii. Atashindwa kusimamia majukumu muhimu ya kiuongozi na kusababisha sinodi kujiona kama si sehemu ya MCT na kutaka kujitenga na sinodi au kujiinua na kudharau uongozi wa MCT kanuni na taratibu za kanisa

ix. Atatumia rasimali za kanisa kinyume na kanuni za fedha au atashindwa kusimamia matumizi mazuri kulingana na kanuni za fedha zilizopo.

x. Atahudumu katika nafasi hiyo kwa muda wa miaka mine na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kama hicho mara moja tu.

D. Taratibu za kumvua Askofu (Askofu mkuu na Askofu wa sinodi) wa MCT

Askofu wa MCT atakayetuhumiwa kwa mambo yaliyotajwa katika fungu la V Ukomo kazi ya Askofu 3, 5,6,7,8 na 9 atavuliwa Uaskofu kwa taratibu zifuatazo:-

1. Baraza la kamati tendaji ya konferensi litaunda tume kuchunguza tuhuma zilizopo
2. Tume itamhoji Askofu huyo na yeyote Yule mwenye taarifa za tuhuma hizo na itampa Askofu husika nafasi hya kujitetea.
3. Tume itaanda taarifa na kupeleka kwenye Baraza maaskofu ambalo litawasilisha hoja ya maandishi kwa kamati tendaji ya MCT ikiambatanisha na taarifa ya tume inayothibitisha tuhuma dhidi ya Askofu huyo na pendekezo ya kumvua Uaskofu.
4. Baraza la kamati tendaji la MCT litajadili tuhuma hizo na mapendekezo ya kumvua uaskofu na kisha kumpa nafasi ya kujitetea.
5. Endapo kamati tendaji itaridhia kwa kura za wazi zaidi ya asilimia hamsinmi (50%)
6. Uamzi wa konferensi kuhusu kumvua uaskofu ni wa mwisho na hautahojiwa na mamlaka nyingine
7. Askofu atakayeacha kazi kutokana na sababu zilizotajwa katika fungu la V ukomo wa Askofu 1,2,10 ataendelea kufanya kazi za kichungaji zisizohusiana na uongozi kwa kadri atakavyoombwa kufanya hivyo.Ataendelea kutunzwa na kanisa hadi pale atakapofariki Dunia .Aidha mjane wa Askofu na watoto wasio zidi umri wa miaka 18 pia wataendelea

kutunzwa na kanisa hadi pale mjane atakapofariki dunia na watoto watakapovuka umri wa miaka 18

D. Utaratibu wa kujaza nafasi ya uaskofu mkuu

Nafasi ikiwa wazi kabla ya kumaliza muda wake

Endapo nafasi ya madaraka ya Askofu mkuu itakuwa wazi kutokana na ,

1.). Askofu mkuu kufariki Dunia

2). Askofu mkuu Kujiuzulu

3). Askofu mkuu kuondolewa uaskofu kwa mujibu wa sheria

Basi baraza la maaskofu watachagua mmoja wao kutoka miongoni mwa maaskofu kukaimu ndani ya miezi sita (6)

Mke wa Askofu wa sinodi

i). Mke wa Askofu wa sinodi ndiye mwangalizi wa idara ya akina mama ngazi ya sinodi akishirikiana na mratibu wa akina mama (wanawake) na idara ya akina mama viongozi wote watashirikiana kuongoza jumuiya hiyo.

ii). Mke wa Askofu wa sinodi ndiye kiongozi mshauri wa wake wa wachungaji anayeweza kuwafundisha malezi na kuwatunza waume zao na watoto wao.

**IBARA YA 17: MCHUNGAJI KIONGOZI**

Mchungaji kiongozi atateuliwa na askofu mkuu wa MCT kutoka miongoni mwa wachungaji wanaosimamia saketi na atakuwa ndiye kiongozi msaidizi wa saketi na atawajibika kwa askofu wa sinodi

1. Mchungaji kiongozi wa saketi atafanya kazi zifuatazo:-
    - A. Kuwa kiongozi wa baraza, la saketi pamoja na vyombo vyake.
    - B. Kufanya kazi zote za kichungaji zilizoainishwa katika fungu la V kazi za mchungaji wa saketi
    - C. Kusimamia utekelezaji wa maamzi yote ya ngazi za juu
    - D. Kuwa mwenyekiti wa baraza la saketi na mkutano wa saketi
    - E. Kutoa taarifa muhimu kwa ngazi za juu kwa mfumo utakao kuwepo
    - F. Kupokea na kutekeleza uamzi wote wa kamati tendaji ya sinodi.\
    - G. Kumjulisha Askofu habari zote za matatizo yatakayojitokeza katika saketi na zaidi ya mambo yote ya kiserikali.
    - H. Kuitisha faragha ya wachungaji katika saketi
    - I. Kusimamia mikutano ya uamsho katika saketi
    - J. Kupanga na kusimamaina mikutano ya uamsho katika saketi

**IBARA YA 18: MCHUNGAJI**

1. Mchungaji ni kiongozi wa MCT mwenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa sifa za kiongozi zilizotajwa ambaye amewekewa mikono na Askofu mkuu katika ibada maalum (ordination) na kupewa cheti cha uchungaji
2. **SIFA ZA MCHUNGAJI**
   i. Mkristo aliye na ushuhuda mzuri na elimu ya msingi na kuendelea amehitimu chuo cha theolojia au chuo cha biblia kinachotambulika na MCT kwa ngazi ya angalau Dipolma
   ii. Mwinjilisti mwenye umri usiopungua miaka 30 na mwenye uzoefu kazini na amekaa katika huduma hiyo kwa muda usiopungu miaka minne (4) ndani ya kanisa la Methodist MCT
   iii. Mwenye ushuhuda wa kutoa fungu la kumi (1/10)
   iv. Awe na mke mmoja na cheti cha Ndoa
   v. Awe na mme mmoja na cheti cha Ndao

3. **Taratibu za kumpata Mchungaji**

Mchungaji atapatikana kwa utaratibu ufuatao:-

A. Ataomba kwenye kanisa la mahali /mtaa
B. Atapigiwa kura za ndiyo na zitapelekwa saketi
C. Saketi watampigia kura kasha watapeleka sinodi
D. Sinodi itamuidhisha kwa kura kasha aidha kwenda kusoma theolojia au kupokelewa kazini na itatokana na sivbi zake.
E. Na mwisho sinodi itampeleka konfaransa kwa mahojiano zaidi

4. **Kazi za mchungaji**

i. Kuwa kiongozi wa kanaisa la mahali
ii. Kufika katika kanisa la mahali lililokatika saketi mara kwa mara

Iii.Kuwatembelea waumini wote wa kanisa apate:-

a. Kuwafahamu

b. Kufariji walio katika taabu kuswashauri na kuwaombea na kuwaonya waliokosa ili warrudi kwa Bwana.

IV. kutoa huduma za kichungaji katika kila kanisa la mahakli lililoko katika saketi

a. Kuhubiri na kufundisha Neno la Mungui
b. Kutoa ibada ya ushirika mtakatifu kutokana na utaratibu wa ibada za MCT
c. Kuomba kwa ajili wakristo na kazi ya Mungu
d. Kuongoza ibada ,Kuongoza ibada wakati Askofu akihudumu kama kiongozi wa saketi hayupo
e. Kufungisha Ndoa za wakristo kwa kufuata utaratibu MCT
f. Kuweka wakfu watoto
g. Kuweka mawe ya msingi katika majengo
h. Kuweka wakfu majengo ya kanisa, kanisa ,nyumba vyombo vya muziki na vitu mbali mbali nk
i. Kufungua majengo
j. Kuzika wafu sawa sawa na utaratibu wa MCT
k. Kuwawekea mikono viongozi wa kanisa la mahali
l. Kushirikiana na mwinhjilisti,wazee a kanisa na mashemasi katika kuwapima wanafunzi wa kateksimo wanaostahili kubatizwa
m. Kuwafundisha wakristo Neno la Mungu kwa njia mabali mbali ili waishi maisha matakatifu na kupendeza Mungu.
n. Kuendesha mikutano ya injili na uamsho na atafuata sheria za Nchi kupitia viongozi wa serikali mahali atakapokuwa.
o. Kuitisha faragha ya wainjilisti, wazee na mashemasi wa kanisa na viongozi wengine wa idara.
p. Kuwafundisha wainjilisti, wazee wa kanisa na viongozi wengine yanayo wahusu utumishi wao kwa kanisa.
q. Kuwajibika kwa mchungaji kiongozi na kwa Askofu wa sinodi
r. Kuongoza baraza la makanisa

s. Mchungaji anapostaafu ataendelea kutunzwa pamoja na familia yake na ikitokea akafariki dunia mamamchungaji atatunzwa na kanisa mpaka atakapofariki.

**IBARA YA 19: MWINJILISTI**

1. Mwinjilisti ni kiongozi wa kanisa la mahali chini ya mchungaji wake, ni mhubiri wa injili anayetambulika na uongozi wa MCT
2. Mwinjilisti akiwa katika kanisa la makao makuu ya saketi atasimamia kazi za siku kwa siku chini ya mchungaji wa saketi.
3. Mwinjilisti pamoja na kuwa na sifa zilizopbainishwa katika ibara ya 16 atakuwa pia na sifa zifuatavyo:-
   A. Awe angalau na elimu ya msingi na kuendelea na ushuhuda mzuri, cheti cha elimu ya Biblia au theolojia kinachotambulika na MCT
   B. Mkristo aliye na ushuhuda mzuri mwenye uwezo wa kufanya kazi ya uinjilisti imani mwenendo wa kikristo awe mwenye umri usiyopungua miaka 20 uaminifu na uvumilivu katika maisha ya kila nsiku.
4. **Kazi za Mwinjilisti**
   i. Kuongoza ibada za kanisa
   ii. Kuhubri nakufundisha Neno la Mungu
   iii. Kuwatembelea wakristo wote apate;
      A. Kuwafahamu
      B. Kuwaona kama wako salama
      C. Kuwafariji na kuwatia moyo katika taabu
      D. Kuwashauri waliokosa ili warudi kwa Bwana
5. Kuwatembelea majirani wasio wakristo hasa walio wagonjwa wahitaji na walio katika taabu apate;
   A. Kuwafahamu
   B. Kuwaombea
   C. Kuwafariji
   D. Kuwasaidia
   E. Kuwashauri
   F. Kuzika wakristo waliokufa

G. Kuhimiza na kusisitiza katiba ,maadili,taratibu na sheria za MCT
H. Kufundisha kateksimo na kuwatayarisha wanafunzi wa kateksimo kwa ushirika kamili wa kanisa.
I. Kusimamisha kazi mzee wa kanisa, shemasi au kiongozi yeyote wa kanisa na nuumini anaye tuhumiwa kukiuka kanuni, taratibu na sheria za MCT.
J. Kuwa mwenyekiti wa baraza la kanisa kama hakuna mchungaji
K. Kuandika na kumpelekea mchungaji taarifa ya kazi zake kila mwezi
L. Kuwajibika kwa mchungaji wa saketi

**IBARA YA 20: MZEE WA KANISA**

Mzee wa kanisa ni kiongozi msaidizi wa mchungaji na mwinjilisti wa saketi na kanisa la mahali aliyechaguliwa na wakristo na kuwekewa mikono na mchungaji

A. Sifa za mzee wa kanisa
   **i.** Kwa mujibu wa (1 **Timotheo 3:1-7)**
   ii. Mtu asiyelaumika
   iii. Mme wa mke moja
   iv. Mwenye kiasi
   v. Mwenye busara
   vi. Mtu wa utaratibu
   vii. Mkaribishaji
   viii. Ajuaye kufundisha
   ix. Si mtu mlevi
   x. Si mpiga watu
   xi. Mpole
   xii. Asiwe mtu wa mabishano
   xiii. Asiwe mtu mwenye kupenda na kutamani fedha ya aibu
   xiv. Mwenye kusimamia nyumaba yake vema
   xv. Ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu
   xvi. Mstahilivu

xvii. Si mtu mwenye kauli mbili Ashuhudiwe mema na watu wa nje
xviii. Mwenye kushika siri ya imani katika dhamiri njema
xix. Mwenye ushuhuda wa kutoa fungu la kumi.

**B. Kazi za mzee wa kanisa**

1. Kumsaidia mchungaji na mwinjilisti wa kanisa la mahali kusimamia maswala yote ya kanisa la mahali
2. Kushirikiana na mchungaji na mwinjilisti katika mchakato wa kuwapima na kuwachagua wanafunzi wa kateksimo wanaostahili kubatizwa.
3. Kushirikiana na mwinjilisti kutembelea wakristo na wasio wakristo
4. Kuongoza ibada za kanisa kulingana na vipawa vyake
5. Kuhubiri na kufundisha Neno la Mungu kulingana na vipawa vyake,ushuhuda wake na elimu yake ya Neno la Mungu
6. Kusimamia katiba ,Maadili ,Taratibu na sheria za kanisa za MCT
7. Kumsaidia mchungaji kugawa mikate na vikombe katika ibada ya ushirika mtakatifu( meza ya Bwana)
8. Kuwa mjumbe wa baraza la saketi
9. Kuwajibika kwa mchungaji na mwinjilisti
10. Kusimamia shughuli mbalimbali za ibada ikiwa ni pamoja na kuhakikisha fedha zinahesabiwa na kukabidhiwa kwa mtunza hazina

**IBARA YA 21: SHEMASI WA KANISA**

Shemasi wa kanisa la Methodist ni kiongozi msaidizi wa mchungaji na mwinjilisti atachaguliuwa na wakristo na kuwekewa mikono na mchungaji

**A. Sifa za shemasi**

1. Kwa mujibu wa (1**Timotheo 3:1-8)**

i. Mtu asiyelaumika
ii. Mme wa mke mmoja au mke wa Mme Mmoja
iii. Mwenye kiasi
iv. Mwenye busara
v. Mtu wa utaratibu
vi. Mkaribishaji
vii. Mtu ajuaye kufundisha
viii. Si mtu mlevi

ix. Si mpiga watu
x. Mpole
xi. Asiwe mtu wa mabishano
xii. Asiwe mtu wa kupenda na kutamani fedha za aibu
xiii. Mwenye kusimamia nyumba yake vema
xiv. Ajuaye kutiisha nyumba yake katika ustahivu
xv. Asiwe mtu aliyeongoka karibuni
xvi. Ashuhudiwe mema na watu wa nje
xvii. Mstahimilivu
xviii. Si mtu wa kauli mbili
xix. Mwenye kuishika siri ya imani katika dhamiri safi

**B. Kazi za shemasi wa kanisa**

1. Kumsaidia mchungaji na mwinjilisti wa kanisa la mahali katika maswala yote ya kanisa hilo
2. Kutunza jengo la kanisa kwa kuangalia usafi wake ,mapambo yake, na matengenezo yake.
3. Kushiriki kuwachagua na kuwatayarisha wanafunzi wa kateksimo wanaostahili kubatizwa
4. Kusimamia katiba, maadili, taratibu na sheria za kanisa na vyombo vyake.
5. Kusimamia shughuli mbali mbali za ibada ikiwa ni pamoja na kuhakikisha utulivu na fedha zinahesabiwa na kukabidhiwa kwa mtunza hazina.

## SEHEMU YA SABA: MABARAZA KURUGENZI NA IDARA

### IBARA YA 22: MKUTANO MKUU WA KONFERENSI

A. Kutakuwa na mabaraza ya uamzi ya MCT kama ilivyo ainishwa kwenye katiba Fungu la VII iliyofanyiwa maboresho Juni 2023

i. Kamati tendaji ya konferensi
ii. Mkutano mkuu wa konferensi
iii. Baraza la maaskofu
iv. Mkutano mkuu wa sinodi
v. Kamati tendaji ya sinodi

## AJENDA ZA SINODI
## SEHEMU YA UWAKILISHI

**ANGALIZO**: Mihtasari ya sinodi wapewe wajumbe katika maandishi na baadae kuambatanishwa na mihtasari ya sinodi.
Katibu wa kamati atawakilisha na kuvipeleka kwenye sinodi itaamua kuwa siyo ya lazima kuchagua mjumbe wa kamati,ambayo ni kazi ya kamati hiyo,kama iliovyoainishwa kwenye ajenda ya kamati,itashughulikiwa wazi kwenye sinodi.( s.o 37) (3)

a. Mahudhurio ya Wajumbe
b. Wajumbe walioomba ruhusa

2. **Kuteua**
   a. Katibu wa sinodi (mchungaji) ,na kama ikipendeza awe mshirika wa kawaida kuwa katibu msaidizi(S.O. 35) Kuchukua ofisi haraka baada ya uchaguizi.
   b. Waandishi wa barua

**Ajenda no. 3.** Kupokea salaama kutokla sehemu mbalimbli

**Ajenda no. 4.** Kuma salaamu kutoka sinmodi klwenda sinodi zingine na konferensi yetu

**Ajenda no. 5. Taarifa ya kazi ya Mungu kutoka Saketi zetui**

**HOTUBA YA ASKOFU WA SINODI**

**YATOKANAYO NA HOTUBA ASKOFU (4) WANNE**

**Kupokea salaam za Askofu Mkuu na kuzungumza na wajumbe wa mkutano mkuu.**

i. Kupokea maoni ya wajumbe ya hotuba ya Askofu mkuu (6) watu sita

**Ajenda no. 6**. (a) Je, kuna mapendekezo yoyte ya kugawanya sinodi au saketi au kanisa la mahali?

( b) Je, kuna makanisa ,mapya yaliyoanzishwa mwake jana?

(c) Je, kuna mapendekezo yoyote ya mikutano ya injili iliyofanyika,na matokeo yake ni yapi?

**Ajenda no. 7.** Mikutano ya saketi na makanisa ya mahali inafanyika kama ilivyopangwa? (wachungaji)

**Ajenda no.8**. Je, kuna mapendekezo yoyote yale yaliyotumwa na konferensi kwenye sinodi ili wajumbe watoe maoni.Kama yapo ni nini maoni ya sinodi?

**Ajenda no**. 9. Je, kuna maamuzi yoyote ambayo saketi zilikaa na kupendekeza kuwa yaletwe kwenye kikao cha sinodi hii? (Wachungaji)

**Ajenda no**. 10. Kama kuna ajenda zinahitajika kushghulikiwa na muongozo wa sinodi basi ziletwa kwa katibu wa sinodi mapema

**Ajenda no**. 11.(a) Taarifa ya kamati tendaji hya sinodi na maamuzi yao juu ya jambo lililojadiliwa na kamati kamalipo liwasilishwe

(b) Kuteua kamati tendaji ya mwake ujao

**Ajenda no. 12. (**a) Takwimu za washirika wote ubatizo kila saketi itoe taarifa zake.

(b) Takwimu za ubatizo zote zinawekwa vizuri na vyeti na orodha ya washirika wote.

(c) Taarifa za kuhama washirika kwenda sehemu nyingine zinatolewa ofisini sawsawa? (Wachungaji na wainjilisti)

**Ajenda no. 13**. Nini kifanyike kuhakikisha wanapatikana wanafunzi kwa ajili ya huduma ya kazi ya Mungu?

**Ajenda no. 14**. Taarifa ya uwakili

(a) Taarifa ya kamati ya uwakili kama imeteuliwa na maamuzi yake juu nya ajenda

**Ajenda no 15**. Mafundisho ya walei

(a) Taarifa ya mafunzo ya walei inayofanyika kjwenye sinodi na watoe taariofa ( wachungaji)

**Ajenda no. 16. Elimu**

(a) Taarifa ya kamati ya elimu aliyeteuliwa atoe taarifa

(b) Uteuzi wa wawakilishi kusimamaia bodi Na teuzi zingine Kama inavyohitajika
(c) Uteuzi wa kamati ya elimu na klatibui wake kama ipo kwenye sinodi.

**Ajenda no. 17.** Uwajibikaji wa Kikristo katika jamii

( a). Taarifa ya uwajibikaji wa Kikristo katika Jamii.

( b). Uteuzi wa kamati ya Kikristo na katibu kama ipo kwenye sinodi na kamati inahitajika katika jamii.

**Ajenda 18. Vijana**

(a) Taarifa ya kamati ya vijana kama imeteuliwa na taarifa zake
(b) Mpangilio kwa ajilimya vijana na tarehe iliyopangwa na konferensi
(c) Uteuzi wa katibu wa vijana sinodi na kmweka hazina na teuzi zingine kama utahitajika
(d) Uteuzi wa kamati ya vijana kama ipo kwenye sinodi

**Ajenda no. 19**. Wahubiri Walei

( a) . Taarifa ya kamati ya wahubiri walei kma itateuliwa na taarifa zao

(b) Uteuzi wa kamati, na katibu wake kama maamuzi ya sinodi itahitaji.

**Ajenda no. 20**. Maandiko na majarida

( a). Taarifa za kamati ya majarida na machapisho kama itateuliwa na taariofa yao.

( b) Uteuzi wa kamati ,katibu wake kwa uamuzi wa kamati ya sinodi

**Ajenda no.21** Jumuiya ya Umoja wa Akina Mama

(a) Taarifa ya umoja ya Akina mama na taaria yao itolewe
(b) Uteuzi wa mwenye kiti wsa Akina mama sindi katibu na mhasibu
(c) Uteuzi wa kamati ya umoja wa Akina mama kama ilivyo katika taaroifa ya kamati ya sinodi inapohitajika

**Ajenda no. 22** Huduma ya Afya

(a) Taarifa ya kamatimya afya kama itateuliwa na taariofa yao

**Ajenda no. 23**. Kamati ya Mipango, Uchumi, Uwekezaji na Maendeleo.

(a) Taarifa ya kamati ya ,Mipangi,Uchiumi,Uwekezaji na Maendeleo
(b) Uteuzi wa kamati ya Mipango,Uchumi,Uwekezaji na Maendeleo

Mhasibu wa sinodi ni mhasibu aliyetoka katika kamati ya Mipango, Uchumi, Uwekezaji na Maendeleo

**Ajenda 24**. Taarifa kutoka kwa kamati ya maandalizi ya sinodi iliyoppita

**Ajenda no. 25.**

( a). Je, kuna vitu vingine wakati wa mapendekezo ya sinodi ya kurejesha mafunzo ya watumishi

( b) Kuna mambo mengine ya kuendeleza watumishi katika sinodi

**Ajenda 26.**

(a) Uchaguzi wa wawakilishi wa (akiba) wa konferensi ijayo pamoja na mabadiliko yaliyofanywa na konferensi iliyopita kwa kura baada ya uteuzi kutoka konferensi
   i. Ambapo itaombwa kuwachagua wawakilishi watatu au zaidi wanaume au wanawake watachaguliwa
   ii. Wagombea wa wawakilishi katika uchaguzi watatangazwa kuwa wagombea kama hakluna wagombea katika uchaguzi huo mgombea lazima achaguliwe
   iii. Wajumbe wa kamati tendaji ya sinodi na makatibu wa sinodi kama hawana nafasi kwenye sinodi watakuwa kama viongozi wastaafu.Uteuzi wa wawakilishi kweneye klamati ya konfrensi kwa uteuzi wa konferensi iajyo wataingia ofisisi katika konferensi iajyo (mchungaji moja na mleo moja)

**Ajenda 2o. 27**. Uchaguzi wa watumishi Walei na Makanisa Mengine watahudhuria sionodi ijayo kifungu hiki kinaweza kuachwa kwa mkamati tenfdaji ya sinodi

**Ajenda 28**. Teuzi zingine kama itakvyopendekezwa

**Ajenda no**, 29. Je, Kuna jambo jingine la kuwasilisha mbele ya sinodi?

**Ajenda no.** 30. Je, kuna kifungu kinachohitaji utelezaji wa sinodi hii, ambacho tunahitaji kuwasilisha kwenye konferensi?

**SEHEMU YA TANO: UTUMISHI NDANI YA KANISA**

(a) Wachungaji waliopo

(b) Wachungaji waliop[ata hudhuriu kutoka kwa Askofu
(c) Je, Kuna asiyehudhuria bila ruhusa ya Askofu?
(d) Kuna ambaye amekwepo kwenye sinodi na konferensi iliyopiuta na bado yuko chini ya sheria ya hii sinodi

**Ajenda no. 31**. Je, kuna mtumishi miongoni anaendelea kumfanya kazi ya huduma kwa uaminifu? Je, anaamini na kuhubiri imani yetu? Je, anatazamia na kuimarisha imani yetu?je, ana uwezo wa ushindani wa kazi yetu?

**Angalizo**: Jina la kila Mchungaji lisomwe kwa kupokezana na atajibu au kwa niaba yake Askofu atamjibia

**Neno**: Imani yetu inajulikana na inalinganishwa na wokovu iliyowekwa na viwango vya kanisa la Methodist? Askofu wa sinodi ataandaa huduma ndogo ya mtihani wa mtu moja moja na kuwekwa wakfu ikilinganmishwa na swali hili.

**Ajenda no. 32.** Wachungaji wangapi walioa toka sinodi iliyopita?

**Ajenda no. 33.** Je, kuna mchunagji aliyefariki toka sinodi ilioyopita? Kama ni hivyo basi kitendo cha kumbukizi kwa ufupi na shukrani itaandaliwa kwa mchungaji aliye farika toka sinodi iliyopita maandika yatosomwa na kuthibitishwa (kanuni)

**Ajenda 34**. Je, kuna mchungaji anayeomba Kuwepo kwenye konferensi ijayo kwa kujirudiarudia? Nini maoni yetu ya konferensi?

**Ajenda 35.** Taarifa juu ya tabia kazi na masomo kwa kila mdahiliwa aliyewekwa na sinodi kupokelewa nakusikilizwa

i. Taarifa kutoka kwa msimamzi wake
ii. Taarifa ya mdahiliwa kutoka kwa katibu wa sinodi
iii. Wadahiliwa namna gani tunawaidhinisha kwa konferensi ili waendelee Na usahili mkwa mwake ujao?
iv. Wadahiliwa wa namna tiunaowathibitisha waende konferensi ili wapokelewe kuwa mmoja wa wachungajki wa konferensi,sinodi inaweza kusaili mdahiliwa na lazima iangalie kazi ya usahili wake.

**Ajenda 36**. Je, konferensi inaruhusu mdahiliwa kuongoza ibada ya sakramenti ya meza ya Bwana?

**Ajenda 37**.( a)  Wanafunzi waliosahiliwa na taariofa muhimu kwao mkujadiliwa je,tutao maoni kwenda konferensi? Kwamba wapokelewe (Kura halali Kwa msailiwa ziandikwe)

(b). Kama mwanafunzi ataidhishwa kwenda konferensi je, sinodi itazingatia kwamba ni lazima afanye mtihani wa stashahada ya thgeolojia na kufaulu wa Afrika Mashariki.

**Ajenda 38.** Je, kuna mengineyo yanayohusu sinodi hii?

(a). Wawakilishi wa sehemu hya sinodi

(b). Kamati tendaji ya sinodi

**Ajenda no. 39**.  (a). Je, kuna sheria iliyopitishwa katika kikao cha wavhungaji wa konferensi na kutumwa kwenda kwenye kikao cha wachungaji wa sinodi?  Nini mapendekezo mapendekezo yao?

(b). Je, kuna mengiuneyo yanayohusishwa na sehemu hii ya sinodi katika konferensi iliyopita?

**Ajenda no. 40**. Taarifa ya kazi ya Mungu

**Ajenda 41.** Je, taarifa zotye za ndoa zinatunzwa katika kila saketi? Na majumuisho yanayotengenezwa kwenda jkwa msajili wa ndoa kama ilivyo tajwa kwenye sheria.

**Ajenda 42**. Je, sehemu hii ina mengineyo ya kuwasilisha kweny:

a. Uwakilishi wa sinodi
b. Kikao cha wachungaji na Maaskofu cha konferensi

**Ajenda no.  43**. Ajenda zilizoletwa na wajumbe kwenye mkutano mkuu wa sinodi

**Ajenda no. 44**. Je kuna mengineyo kabla ya sinodi hii?

**MABARAZA YA SAKETI**

**AJENDA ZA BARAZA LA SAKETI**

1. Kikao kifanhywe mwezi wa Pili,Tano,Nane, Kumi na Moja
2. Kikao cha mwezi wa pili kifanyike kabla ya mkutano wa sinodi kukamiliasha maandalizi  ya sinodi
3. Katika ajenda vifungu vilivyoainishwa ndivyo vya kuzingatiwa kwenye mkutano,vifungu visivyoainishwa vizingatiwe kqenye kila kiao
   (a). Mahudhurio: Hudhuru kwa wasiyohuidhuria

(b) Kusoma mhiutasari wa kikao kilicho pita

( c) Yatokanayo na mhutasari na siyo vinginevy visivyo husishiana na ajenda

4. (a). Taarifa ya kazi ya Mungu

   ( b). Mwezi Feb. i. mwakilisho ya kila mshirika katika kilka saketi kulingana na ratiba ya klonferensi

   ii. Je, kuna hatua stahiki zinazochukuliwa kuhakikisha kwamba taariofa ya kumuondoa nakuham,isha mshirika yanatumwa kwenda saketi wanakotaka?

   iii. Je, kuna hatua stahiki zinachukuliwa kuwakaribisha washirika wapya wa Methodist wanaotoka kwenye saketi zingine na kuwasaidia kuhakikisha wanakaribishwa kanisa?Wachungaji,wainjilisti)

   iv. Ni hatu zipi zinazo chukuliwa za huduma za kikuhani kwa watoto wanaopokelewa kanisani na watoto wachanga wanao batizwa?

   v. Ni hatua nzipi inachukuliwa za huduma za kikuhani kwenda hospitalini namagereza ndani ya saketi?

   vi. Mapendekezo ya kuyfungua maeneo ya mahubiri mapaya katika saketi au kufyunga yaliyopo?

   vii. Mwezi Feb.( a) Tunawezaje kutengeneza kazi ya uinjilisti wa saketi hii? Chini ya Mungu ili ifanye zaidi?

   ( b).Ni kazi gani ya uinjilisti utakao chukuliwa

   (c) Mwezi Feb. Ni maboresho yapi au mikutano muhimu iliyopangwa kwa mwake huu?

**Ajenda no. 4**. (a) Taarifa ya fedha ya mhasibu wa saketi (nakala yantaarifa itumwe kila robo ya mwake kwenda bkwa Askofu wa sinodi na kuwasiilishwa kwa Askofu Mkuu)

(b) Mwezi April. Ikipendeza teua kamati ili kumfanya uteuzi kwenye robo ya mkutano kuchagua viongozi wa saketi
(c) Mwezi Oktoba, tathmini ya mapato na matumizi kwa m waka ujao.
(d) Mwezi Nov. maandalizi ya kukaribisha ijumaa kuu na madai ya katibu
(e) Mwezi Nov. Uteuzi wa kamati ya fedha
(f) Mswezi Agost.Taaroifa ya pango la wachungaji nawainjilisti walioko chini ya saketi

**Ajenda no. 5. (**a) Mwezi Nov. Je kuna mengineyo yanayoletwa kwenye kikao kinachohusishwa na mhutasari wakonferensi uliyopita?

( b) Mwezi Feb. Ni ziara zipi zilizofanywa na Askofu wa sinodi au Askofu mkuu kwenye saketii hii?

( c) Mwezio wa Tano. Je, kuna mengineyo yanayopaswa kujadiliwa kwenye mkutano huu Kutokana na mhtasari wa mkutano mkuu wa sinodi uliyopita?

**Ajenda no. 6.** (a) Uthibitisho wa wainjilisti kwa maoni ya mkutano wa wainjilisti kupokelewa kwenye huduma

( b) Maandalizi kwa huduma ya utambulisho kwa wale wainjilisti wapya

( c) Je, kuna maengineyo kwenye mkutano huiu nyaliyoletwa na mkutano wa wainjilisti?

**Ajenda no. 7.(** a)Mwezi Nov. Ni utaratibu wa saketi kuwapeleka walei kwenye mafunzo mwake ujao,program hii lazima ihusishe mafunzo kwa wahubiri .vijana na umoja wa akina mama.

(b)Mwezi Mei .nini kifanyike kuwarudisha nyumbani washirika wetu waliyombali na Mungu na huduma za Kikristo?

**(c)Nini tarajio letu la kuwatia moyo viongozi wa saketi?**

**Ajenda no. 8**.(a) Udhihirisho wa kuteua wanafunzi wanahitaji kuingia katika huduma ya uchungaji,(Kura lazima zichukuliwe na idadi kamili ya ziandikwe)

**Ajenda no. 9. (a**) Je, kuna mazoezi ya wageni shuleni na kwenye zahanati yanafanyika?

( b) Ni jinsi tunaweza kuifanya mazoezi ya huduma ya kichungaji katika shule na tasisi zingine kwenye saketi?

**Ajenda no 10.** a) Taarifa ya idara ya viajana na maelekezo ya mfukoi wa fedaha za vijana na majadiliano yanayohusu vijana

b) Maandalizi ya mafundisho ya j. pili ya vijana na mikusnayiko yao

c) Nov. Uteuzi wa bnaraza la saketi la viajana mwenye kiti,katibu wa viajan na mhasibu katika bartaza la uchaguzi la vijana

**Ajenda no. 11**. a) Taarifa ya Akina mama saketi,na taarifa ya fedha ya akina mama saketi na mjadala juu ya kazi yao.

b) Nov. uchaguzi wa kamati ya akina mama mwenye wa akina mama saketi,katibu na mhasibu kwenye uhaguzi wa kamati ya akina mama

**Ajenda no.11**. Taarifa ya kamati za huduma jamii ya kanisa Kama ipo (wachungaji)

**Ajenda no. 12. Je**, kuna taarifa kutoka kwenye kikao cha kituo Ndani ya saketi?

**Ajenda no. 13. Agost**. Maandalizi ya jumapili ya kuwatazama wagonjwa hiospitalini kwenye saketi

**Ajenda no. 14. Feb**. a) Uchaguzi wa wawakilishi kwenye kamati ya sinodi

(Kiongozi moja na mwakilishi wa walei)

b) Uchaguzi wa wawakilishi kwenye kamati ya sinodi ijayo amabapo sinodi itafanya maamuzi kuwateua (mtumishi moja au mlei kwa kila kamati)

i) Uchumi na mali ii) Uwajibikaji wa wakristo kijamii,iii) wahubirijni walei iv) Maandiko na machapisho v) Umoja wa wanawake vi) Vijana vii) Afya vii) Elimu

**Anaglizo**: Mshirika mmoja wa kamati ya sinodi atamkabidhi mjumbe kiti kwenye sinodi.

i) Feb. Maombi kwenda sinodi kwa ajili ya kuomba ruhusa ya konferensi kununua au kupata ardhi au kununua au kujenga majumba ya moja kwa moja ( taarifa ya mtaalam lazima iwakilishwe katika kila jambo)
ii) Feb. Je, huu mkutano wa robo lina jambo la kuleta mbele ya sinodi?

**Ajenda no 15.** Nov. Kuteuliwa kwa mjumbe moja kwa robo mwaka kama katibu wa mkutano

**Ajenda no .16.** Nov. Maandalizi ya huduma ya maagano kwenye saketi januari mwakani.

**Ajenda no 17**. Nov. Uteuzi wa watumishi wa saketi walei (wainjilisti) kama yupo,kwa mwake ujao.(kifungu hiki kinaweza kuzingatiwa kwa robo zingine,kama hitaji litajitokeza.

**Ajenda no. 18.** Tarehe,Muda na mahali pa m,kutano ujao.

**Ajenda no. 19.** Mengineyo

vi. Baraza la saketi
vii. Mkutanio mkuu wa kanisa la mahali

B. Mabaraza yote haya yataidhinishwa na mkutano mkuu wa konfaransa ambao utafanyika mara moja kwa mwaka na ndio wenye uamzi wa mwisho katika kanisa la MCT
   1. Kanuni hizi zinaelekeza kwamba mkutano mkuu utafanyika mara moja kwa mwaka
   2. Wakati wowote inapotokea dharura
   3. Dondoo (Agenda) za mkutano mkuu wa konfaransa wa MCT zitaanzishwa kwenye kanuni za uendeshaji

**C. Kazi za mkutano mkuu wa konferensi**
   1. Kumchgua Askofu mkuu
   2. Kumchagua Askofu  sinodi
   3. Kuteua na kuidhinisha wadhamini wa mali za kanisa
   4. Kupitisha katiba na kanuni za MCT
   5. Kupitisha sera na kanuni za sheria
   6. Kumthibitisha katibu mkuu
   7. Kuidhinisha uanzishwaji na uzinduzi wa sinodi mpya
   8. Kukasimu shughuli za kanisa kwa mhasibu wa konferensi zenye umuhimi au kuhatarisha uhai wa kanisa
   9. Kupokea taarifa ya utendaji wa kila mwaka

**IBARA YA 23; KAMATI TENDAJI YA KONFERENSI**

Kamati tendaji ya konferensi ni baraza la juu litakalosimamia utekelezaji za shughuli zote za kanisa chini ya mkutano mkuu wa konferensi na Askofu mkuu.

1. Wajumbe wa kamati tendaji
   a. Askofu mkuu (mwenyekiti)
   b. Maaskofu wote wa sinodi
   c. Katibu  mkuu wa MCT
   d. Katibu wa sinodi
   e. Wenye viti wa idara za MCT
   f. Mwanasheria (mshauri)
   g. Maaskofu waliostaafu (wajumbe wa kukaribishwa)
   h. Mtunza hazina  wa sinodi
2. **Kazi za kamati tendaji ya konferensi**
   i. Kumchagua katibu mkuu

ii. Kusimamia sera, kanuni na maadili ya MCT kuhakikisha kuwa maagizo ya konfaransa yanatimizwa katika makanisa yote ta MCT pamoja na idara zake.
iii. Kuteua majina ya mwenyekiti na wajumbe wa kamati Bodi za kurugenzi na idara.
iv. Kupitisha viwango vya mawasilisho ya fedha za kanisa
v. Kusimamia shughuli za uendeshaji
vi. Kuwachagua na kuwateua wajumbe wa kamati ya katiba
vii. Kuweka katiba na misioni
viii. Kisisitiza mikataba na misioni au mashirika yanayohitaji kushirikiana na MCT
ix. Kujadili na kupitisha uanzishwaji na usajili wa taasisi au chombo au kampuni kwa ajili ya uendeshaji wa miradi au shughuli za kiuchumi na kijamii ndani ya MCT
x. Kupokea taarifa za kanisa zima za kila mwaka kwa niaba ya konferensi na kutuma taarifa hizo serikalini.
xi. Kupendekeza tarehe za konferensi
xii. Kujadili fomu za maombi zilizojazwa na wamisionari na wanaoomba kufanya kazi na MCT kusimamia mikataba yao baada ya kukubaliwa
xiii. Kuwatuma wamisionari
xiv. Kusisitiza mikataba ya wamisionari kwa kushirikiana na mission iliyowatuma endapo mmisioni atakiuka imani, katiba,sera kanuni na taratibu za MCT
xv. Kusitisha mkataba na mmisionari atakayekiuka sheria za Nchi.

**IBARA YA 24: BARAZA LA MAASKOFU**

1. Baraza la maaskofu litakuawa ni chombo kitakachosimamia na kumshauri Askofu Mkuu katika mambo ya Imani, maono na utume na madhumuni ya kanisa pamoja na mahusiano ya ndani ya kanisa ya Nchi ya Tanzania.

A. Wajumbe wa baraza la maaskofu

i..Askofu mwenyekiti

ii. Maaskofu wa sinodi

Iii.Maaskofu wote wastaafu

iv.Mwalikwa

V.Katibu mkuu (Hana kura)

B. **Kazi za baraza la Maaskofu**

1. Kupokea taarifa kuhusiana na mambo yote ya imani misioni na mahusiano na kuzishughulikia,

2. Kumshauri Askofu mkuu juu ya maono, utume na madhumuni ya kanisa

3. Kupendekeza maelekezo yatakayosimamia mahusiano kati ya kanisa na madhehebu mengine ya kikristo na yasiyo ya kikristo ndani na nje ya Tanzania

4. Kutoa ushauri kwa Askofu mkuu jinsi ya kuimarisha imani na mshikamano ndani ya kanisa

5. Kuchagua Askofu mkuu wa muda wakati inapotokea tatizo lolote kwa Askofu Mkuu

6. Kupendekeza tarehe za mikutano ya faragha za maaskofu na maudhui yake katika mkutano wa kwanza kila mwaka

7. Kuandaa ushauri wa kutoa kwa Serikali, vyama vya siasa na vikundi vingine unaolenga kudumisha usalama wa Taifa na kudumisha Amani ya nchi

8. Kutatua migogoro ya kiroho na utawala ndani ya kanisa kwa kuteua kamati itakayoshughulikia utatuzi wa migogoro inayotoka nje ya kanisa au iliyokatiwa rufaa na mamlaka nje ya kanisa

9. Kupendekeza kamati ya maadili na nidhamu zitakazoshughulikia wachungaji ikiongozwa na Askofu na nyingine kwa ajili ya walei watakaoshughulikiwa kwa mujibu wa sheria za nchi (Viongozi wawajibikaji makao makuu ya sinodi) makatibu na katibu mkuu

10. Kuwatuma wachungaji wanaofuzu kozi ya uchungaji

11. Kuwahamisha wachungaji toka sinodi moja kwenda sinodi nyingine

12. Kumwondoa au kumrudisha mchungaji kazini

13. Kuwatuma wainjilisti wanaohitimu vyuo vya Biblia na Theologia

**IBARA YA 25: MKUTANO MKUU WA SINODI**

A: Kutakuwa na mkutano mkuu wa sinodi utakaofanyika mara moja kwa mwaka na wajumbe wa mkutano huo ni kama ifuatavyo:-

1: Askofu wa sinodi (Mwenyekiti)

2: Katibu –(Katibu)

3: Mhasibu

4: Wachungaji wote walioko kazini na wastaafu

5: Makatibu wa saketi zote

6: Wahasibu wa saketi zote

7: Wajumbe watakaochaguliwa na ofisi ya sinodi

8: Katibu, Mwenyekiti, na Mhasibu wazee saketi

9: Mwenyekiti Katibu, na Mhasibu akina mama saketi

10: Mweneyekiti, katibu na mhasibu vijana saketi

11. Mwenyuekiti,katibu na mhasibu wa mama sinodi
12. Mwenye kiti,katibu na mahasibu wazee ngazi ya sinodi
13. Mwenyekiti ,katibu na mhasibu viajana ngazi ya sinodi
14. Viongozi wa idara zilizoko sinodi
15. Mwinjilisti mmoja kutoka kila saketi atakayechaguliwa na ofisi ya sinodi

**B. Kazi za mkutano mkuu wa sinodi**

1. Kusimamia utekelezaji wa uamzi wa konferensi na MCT
2. Kusimamia sera ,sheria na kanuni za MCT

3. Kukata shauri juu ya yanayoletwa na kila juu ya mambo yanayohusu sinodi hiyo yanayoletwa na kila baraza la saketi katika sinodi
4. Kuchagua katibu wa sinodi
5. Kupitisha maelekezo ya marekebisho ya katiba ya MCT ngazi ya sinodi kwenda kamati tendaji ya konferensi
6. Kuchagua mhasibu wa sinodi
7. Kupendekeza kwa konferensi kuanzishwa kwa sinodi mpya
8. Kukasimu utekelezaji wa shughuli za sinodi na kamati tendaji ya sinodi

**IBARA YA 26: KAMATI TENDAJI YA SINODI**

Baraza la kamati tendaji ya sinodi ni baraza linalosimamia utekelezaji wa shughuli zote za sinodi na kufuatilia utekelezaji kwa niaba ya konferensi.Na na inapotokea dharura.

A. Wajumbe wa kamati tendaji ya sinodi

i. Askofu wa sinodi (mwenyekiti)

Ii.Katibu wa sinodi (katibu)

Iii.Mhasibu wa sinodi (mhasibu)

Iv.Makatibu wote wa saketi

V.Maaskofu wastaafu wote

Vi.Wachungaji wote

vii.Mweneyekiti, katibu na mhasibu vijana saketi

viii.Mwenyekiti, katibu na mhasibu wazee saketi

ix.Mwenyekiti, katibu na mhasibu akina mama saketi

x. Mwinjilisti mmoja kutoka saketi

Xi.Wajumbe wa bodi ya wadhamini MCT

Xii.Jumuiya ya wanawake Mwenye kiti, katibu na mhasibu

Xiii.Jumuiya ya wanaume, mweneyekiti, katibu na mhasibu MCT

Xiv.Jumuiya ya vijana mweneyekiti, Katibu na mhasibu MCT

Xv.Waratibu wa idara za sinodi

## B. KAZI ZA KAMATI TENDAJI

1. Kutayarisha agenda za sinodi kuangalia matoleo ya makanisa na kuwahimiza wachungaji na wainjilisti, wazee wa makanisa na mashemasi,ili nao wahimize wakristo wamtolee Mungu matoleo kusudi kazi ya Bwana iendelee hadi kufika sehemu mpya ambako Mungu anaruhusu kanisa lifanye kazi yake
2. Kuwatuma waijilisti wanaotumwa na konferensi katika sinodi pamoja na wachungaji
3. Kuwahimiza wachungaji na wainjilisti katika saketi
4. Kuweka na kuainisha mipaka ya saketi
5. Kushughulikia migogoro kwenye saketi
6. Kuwaajiri waratibu na wataalam wengine chini ya mamlaka ya sinodi pamoja na kuwaondoa kazini inpolazimika kwa mujibu wa taratibu za MCT
7. Kupendekeza majina ya wachungaji na wainjilisti yatakayopelekwa kwenye kamati tendaji ya konferensi
8. Kusimamia mali za MCT
9. Kupendekeza tarehe ya mikutano wa sinodi
10. Kumuondoa kazini mwinjilisti aliyetumwa endapo ameshindwa kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa taratibu za MCT
11. Kuwateua wenye viti wa idara na kupitisha majina ya wajumbe wa idara na taasisi/kampuni ya uzalishaji na uendeshaji miradi na shughuli za kiuchumi, na kiamii ndani ya sinodi

### IBARA YA 27: BARAZA LA SAKETI

1. Baraza la saketi ni baraza la juu katika saketi litakaa mara mbili kwa mwaka
   A. Wajumbe ww baraza la saketi

      i). Mchungaji kiongozi wa saketi (mwenyekiti)

      ii). Katibu wa saketi (katibu)

      iii). Mhasibu wa saket

iv). Mzee wa kanisa

v). Katibu wa kanisa

vi). Mhasibu wa kanisa.

vii). Viongozi wa idara zote kutoka kila kanisa

2. **KAZI ZA BARAZA LA SAKETI**

A. Kusimamia na kuendesha mikutano ya kiroho katika saketi
B. Kupokea mambo yaliyoshindikana katika mabaraza ya saketi na kuyachunguza ili kufikia uamzi wa kuyawasilisha ngazi za juu.
C. Kuamua matatizo ya Ndoa kutoka katika mabaraza ya makanisa
D. Kupendekeza au kugawanya kwa saketi katika mabaraza kamati tendaji ya sinodi
E. Kuandaa ibada ya kuwawekea mikono watumishi walioko kwenye saketi
F. Kuhimiza matoleo na mawasilisho katika makanisa yote yaliyomo katika saketi
G. Kubuni na kufikiria mipango na kuanzisha miradi ya kuendeleza makanisa katika saketi
H. Kuhamasisha vijana kujiunga katika vyuo vya biblia
I. Kushughulikia uhamisho wa wainjilisti kutoka saketi moja kwenda saketi nyingine katika sinodi hiyo
J. Kupitisha taarifa za kazi za saketi na kutoa ushauri katika mambo yanayohitaji kuimarishwa
K. Kuhakikisha saketi ina ofisi imayofahamika

**IBARA YA 28: BARAZA LA KANISA LA MAHALI**

Baraza la kanisa la mahali au mtaa ni baraza la juu kaatika kanisa la mahali/mtaa

**A. Wajumbe wa baraza la mahali/mtaa**

i.Mchungaji /Mwinjilisti (mweye kiti)
Ii.Wazee wa kanisa
Iii.Katibu wa kanisa
Iv.Mhasibu wa kanisa
V.Shemasi wa kanisa

Vi.Viongozi wote wa idara (vijana, wazee, wanawake)
vii Viongozi wengine waliyomo

**B. KAZI ZA BARAZA LA MAHALI**

I.Kuandaa ibada za kikanisa

ii.Kuwalinda, kuwalea na kuwafundisha wakristo waendelee kukua katika ukristo wa kweli

Iii.Kufikisha huduma za kiroho na za kimwili kwa wakristo wote na kwa majirani.

Iv.Kujadili  matatizo yanayotokea kanisani na kutoa uamzi kwa yale yaliyo ndani ya uwezo wa baraza la kanisa la mahal yanayoshindikana yapelekwe baraza la saketi

V.Kuhimiza na kukusanya matoleo na kuyapeleka kwa mhasibu wa saketi

Vi.Kukazia na kusimamia katiba sheria, maadili na mafundisho ya MCT

Vii.Kuhakikisha kwaya zinahudumu zenye maadili ya MCT na kuzichukulia hatua

pale zinapopotoka au kukengeuka

Viii.Kupenedekeza kwa baraza la saketi sehemu ambayo panafaa kuanzisha kanisa

ix.Kusimamia na kuratibu ujenzi na kutunza jengo la kanisa,nyumba ya ,mchungaji( Mwinjilisti,kiwanja ,miti,mali,fedha na vitu vyote vya kanisa)

X.Kubuni kufikiria mipango na kuanzisha miradi ya kanisa ya maendeleo

Xi.Kutoa taarifa ya kazi za kanisa la mtaa kwa baraza la saketi

xii. Kutoa taarifa za kamati mbali mbali zilizo chini ya baraza la kanisa la mahali na kudhibiti shughuli za kamati hizo

Xiii.Kuwaanda vijana wawe tayari kujiunga katika vyuo vya biblia na theolojia.

A. Kanuni hizi zinaelekeza kwa wajumbe halali wa vikao kila wakati na kushiriki kikamilifu endapo mjumbe atakosa kuhudhuria kikao kinachmhusu mara tatu bila taarifa atakua amejifuta ujumbe kwa utoro wake, mwenyekiti,mjumbe aliyejifuta kwa utoro wake,haruhusiwi kuchaguliwa kwenye nafasi yeyote ya ngazi yeyote hadi baada ya kupita awamu moja ya utawala.
B. Wajumbe halali wa kikao husika wanakaribishwa na katibu wa kikao kwa maandishi yenye mwaliko orodha ya agenda,mahali pa kikao,muda wa wiki wa vikao,utazingatia muda wa siku zisizopungua 14.kwa wajumbe kufika na kuhudhuria vikao
C. Vikao vyote vitaitwa na katibu wa vikao akishirtikiana na mwenyekiti. Kikao kitakua halali ikiwa kina akidi (quoram ) ya angalau 50% ya wajumbe halali wa kikao husika
D. Mkutano mkuu maalum wa kurekebisha katiba utapaswa kuwa na akidi ya asilimia sabini na tano 75% ya wajumbe halali wa kikao hicho na kura zinaweza kupitisha marekebisho ya katiba ni asilimia sabini na tano 75% ya kura halali zilizopigwa.
E. Kikao kitaendeshwa na mwenye kiti husika na katibu husika.Endapo mweneyekiti hayupo kwa taarifa, Kikao halali kilichoitishwa kitafanyika kwa kuendeshwa na mmoja wa wajumbe watakaomchagua.
F. Maamuzi mengine ya vikao(visivyo mkutano mkuu wa MCT wa kurkebisaha katiba) yanapigiwa kura yatapitishwa kwa wingi wa kura .Endapo kura zitalingana mwenyekiti wa kiako husika atapiga kura ya uamzi
G. Maamuzi yahusuyo viongozi mbalimbali yatafiuata maelekezo yaliyotolewa kwenye vikao vya ngazi ya juu husika.
H. Kanuni hizi zinasisitiza makatibu wa vikao kuandika mihutasari ya vikao vyote si ya zaidi ya wikimbili tangu tarehe ya vikao.Aidha katibu atatunza na kuwasilisha mihutasari na taarifa za utekelezaji wake kwenye vikao vinavyofuata kwa ajili ya kuthibitishwa na kujadili taarifa za utekelezaji.

**IBARA YA 29: IDARA YA HUDUMA ZA KIROHO**

A. Idarta ya  Uinjilisti na Umisheni ambayo itajikita katika uenezaji wa Neno la Mungu,Uanzishwaji wa makanisa  na kusimamia misheni zilizopo  na zitakazoanzishwa .Itafanya kazi kwa karibu na wamisionari kwa lengo la kueneza injili ya Neno la Mungu.

**B. Idara ya elimu ya kiristo itajumuisha kutoa elimu kwa makundi yote yaliyomo kanisani kama vile :-**

i.Wanaume
ii.Wanawake
iii.Watoto
Iv.Viongozi watumishi wa MCT
V.Uandaaji wa mtaala ya kufundishia masomo ya biblia katika vyuo vya biblia
vi. Uandishi wa vitabu

**C. Idara ya Mafunzo ya Biblia na Theolojia**

a. Itahusika na ufundishaji wa masomo ya biblia katika vyuo vya biblia
b. Uandishi wa vitabu
c. Utafiti  wa masomo ya biblia

**D. Idara ya uimbaji ,kwaya  na  muziki**

a. Kusimamia na kufundisha nyimbo za tenzi zinazoimbwa kanisani MCT
b. Kuhakikisha nyimbo zinazoimbwa za kwaya zinaleta utukufu kwa Mungu
c. Kuhakikisha kwaya zote ziwe na nidhamu za kutosha na zivae mavazi ya heshima
d. Kuanzisha makongamano ya kwaya.

**E. Idara ya Ibada ,Maombi na Maombezi**

1. Kanuni hizi zinatambua huduma mbili za kiroho na kimwili zitolewazo na MCTkwa msaada wa Roho mtakatifu huduma hizo zinapaswa kutolewa kwa mujibu wa katiba ya MCT na kanuni zake.
2. Kanuni hizi zinaelekeza kufanyika kwa ibada kama zilivyoelekezwa katika katiba ya MCT (Kanuni ya 17) ambayo panatajwa ibada ya jumatano, jumapili na sikuu. Siku zingine zilizo katka mpango wa kanisa na

maombezi kwa kufuata utaratibu wa ibada za MCT inatumika.

3. Kanuni hizi zinamkataza mchungaji /mwinjilisti/kiongozi muumini yeyote kuanzisha na kuongoza ibada za kanisa kinyume cha taratibu za ibada za Methodist church in Tanzania (MCT) kwa kufanya hivyo ni uasi anapaswa kuchukuliwa hatua za kinidhamu.
4. Kanuni hizi zinaelekeza menejimenti ya kanisa katika kila ngazi husika kuhakikisha kuwa viongozi waliowekewa mikono  maaskofu,wachungaji, na viongozi wa ibada wanaeleimisha ipasavyo juu ya taratibu za uendeshaji wa ibada inavyopaswa kwa mfano (sare)Aidha vyuo vya biblia/theolojia na umisheni na program za masomo ya muda mfupi na mrefu yanayoendeshwa  ndani ya MCT vewe  na mada  na utaratibu wa uendeshwaji wa ibada na tafsiri sahihi ya biblia kwa kuzingati muktadha za maandiko na pia fasihi ya mwandishi iliyotumika.

E.**Sakramenti**

Kanuni hizi zinatambua kuwa maaskofu na wachungaji wana mamlaka ya utoaji wa huduma za sakramenti ambazo ni:-

a. Ubatizo
b. Meza ya Bwana  (Ushirika Mtakatifu)
c. Ndoa
d. Kuweka wakfu watoto
e. Kuwapokea waumini wapya
f. Kuwawekea mikono wachunagji

6. Kanuni hizi zinasisitiza kuwa mwongozo wa taratibu za ibada ya kanisa la MCT ifuatwe katika utoaji wa huduma za sakramenti hizi.

## IBARA YA 30: IDARA YA HUDUMA ZA KANISA

1. Kanuni hizi zinatambua kuwa katika kanisa la MCT kuna muundo wa uongozi wa idara zinazotekeleza majukumu mbali mbali ili kutimiza

madhumuni ya MCT  rejea katika katiba ya MCT Fungu la VII ukurasa wa 88 -150

a. Idara ya rasimali watu
b. Idara ya uinjilisti na umishenari
c. Elimu ya kikiristo
d. Mafunzo ya biblia na theolojia
e. Uimbaji kwaya na muziki
f. Idara ya wanawake
g. Idara ya wanaume
h. Idara ya vijana
i. Idara ya miradi
j. Idara ya walemavu
k. Idara ya Sunday school
l. Idara ya watoto

A. Kuratibu mipango ya muda mfupi na program za kazi za kiroho kwa ajili ya kuidhinisha utekelezaji wake.
B. Kuanzisha mafunzo ya kimataifa kwa kanisa la MCT kwa mwaka na kusimamia utekelezaji wake.
C. Kushauriana  na katibu mkuu na waratibu wa saketi kuhusu kupata maeneo ya kuanzisha huduma za kiroho kama vile: maeneo ya kujenga na kuendeleza vyuo vya biblia na kufanya mikutano ya injili
D. Kutoa taarifa za utekelezaji wa program na mipango ya kiroho katika menejimenti ya kamati tendaji ya MCT
E. Kutathmini utendaji wa vitengo vyote na program za huduma za kiroho
F. Kusimamia mafunzo ya aina zote yahusuyo Neno la Mungu vyuo vya Biblia na theolojia
G. Kuratibu semina mbali mbali za mafundish ya Neno la Mungu ndani ya MCT pamoja na kozi za uinjilisti na uchungaji
H. Kusimamia na kutetea msimamo wa mafundisho sahihi (Doctrines) ya MCT dhidi ya mafundisho potofu na kutafuta uso wa  Bwana
I. Kuandaa mtaala wa kufundisha Neno la Mungu makanisani na mashuleni
J. Kuhakiki na kupima usahihi wa mafundisho kwa kila kanisa la mahali/kijiji
K. Kusimamia vitabu vinavyo[pitishwa na mabaraza kama miongozo ya kufundishia Neno la Mungu
L. Kufanya kazi nyingine inayopangiwa na kamati tendaji ya konferensi.

C. Kazi za idara za MCT

1. Idara ya wanawake itahusiuka kwa kuwahudumia wanawake na kuwahudumia wanawake wahitaji kiuchumi kutoa misaada,kuwawezesha katika kazi za kijamii
2. Idara ya wanawake itahusika na kuwahudumia wanaume wahitaji katika huduma za kijamii ,kiuchumi na kutoa misaada na kuwawezesha katika kazi zao za kujitafutia
3. Idara ya vijana itahusika na kuwawezesha vijana wahitaji kiuchumi,kutoa misaada katika shughuli za kujitafutia
4. Idara ya watoto itahusika na misaada kwa watoto wenye mazingira magumu kwa kuwalea na kuwajali
5. Idara ya walemavu inahusika na kuwasaidia walemavu katika shughuli za kiuchumi na kutoa misaada ya kurahisisha maisha yao

## IBARA YA 31: IDARA YA KURUGRENZI YA MIPANGO, UCHUMI UWEKEZAJI NA MAENDELEO

A. Kurugenzi ya mipango ,uchumi, uwekezaji na maendeleo itakuwa na idara zifuiatazo:-

1. Idara ya uchumi na uwekezaji itahusika na.
   a. Kusimamia uendeshaji wa miradi mbali mbali za kibiashara itakayoanzishwa ikiwa ni kampuni au ubia au muundo wowote utakaidhinishwa
   b. Kufuatilia usajili kwenye mamlaka husika za serikali taasisi au kampuni za uwekezaji na uendeshaji wa miradi au shughuli za kiuchumi na kijamii chini ya MCT
   c. Kutekeleza mipango ya muda mrefu na muda mfupi ya kanisa ikiwemo ujenzi na uendeshaji wa shule ,vyuo,zahanati,hospitali,vituo vya afya na mengineyo aidha kupitia hospitali na vituo vya afya vya kanisa idara itahakikisha huduma za afya zinatolewa kwa ubora stahiki.
2. Idara ya Mipango na Maendeleo itahusika na:-
   a. Kubuni kisha kushauriana na katibu mkuu,waratibu wa mpango wa sinodi na saketi juu ya,upatikanaji wa maeneo ya kuwekeza miradi

ya kanisa ikiwemo ujenzi wa makanisa,shule,vyuo,zahanati,hospitali vituo vya afya.

b. Kuandaa mipango na mikakati ya muda mrefu na muda mfupi na program za kazi za MCT
c. Kutathmini hali ya uendeshaji wa miradi idara za usimamizi na kushirikiana na mkurugenzi.

Kazi za kurugenzi ya mipango uwekezaji, uchumi na maendeleo ni pamoja na zifuatazo:-

1. Kuratibu, mipango, mikakati ya muda mrefu na mfupi na program za kazi za MCT kwa ajili ya kuidhinishwa na kusimamia utekelezaji wake kupitia idara husika.
2. Kubuni na kusimamai utekelezaji wa miradi ya kanisa na uanzishaji miradi.
3. Kushauriana na katibu mkuu waratibu wa mipango uchumi na utawala wa sinodi upatikanaji wa maeneo ya kuwekeza miradi ya kanisa na ujenzi wa kanisa.
4. Kutoa taarifa za uchumi na uwekezaji katika kamati tendaji ya konferensi.
5. Kutathmini uendeshaji wa miradi ya idara za usimamizi na kushauriana na viongozi wa bodi na kamati husika.
6. Kushughulikia usajili kwenye mamlaka husika za serikali na taasisi na uendeshaji wa miradi au shughuli za kiuchumi na kijamii chini ya MCT

**3. Uchumi na Maendeleo**

1. Kanuni hizi zinatambua na kusisitiza utoaji wa huduma kamilifu katika Nyanja mbali mbali na nyinginezo kupitia idara mbali mbali Jumuiya,Taasisi,Idara Asasi program na miradi ya kanisa kutoa huduma za afya ndani ya kanisa elimu,uchumi endelevu ustawi wa maendeleo ya jamii,mawasiliano na misaada mbali mbali kwa wahitaji
2. Kanuni hizo zinaagiza kuwa huduma hizo zifuate mwongozo na maelekezo ya wizara husika za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
3. Kanuni hizi zinaagiza mamalaka katika ngazi zote za kanisa kuibua, kuanzisha, kuratibu na kuendesha huduma tajwa katika kanisa kwa nguvu zote kwa kutumia wataalamu wa ndani na nje ya MCT.
4. Kanuni hizi zinakumbusha kuwa kanisa lililo imara ni lile linalokuwa kiroho na kimwili ili iweze kuwahudumia waumini wake.Kwani dini iliyo safi mbele za Mungu ni kuwahudumia wahitaji (**Yakobo 1:26-27**) Hivyo kanuni

zinaelekeza kamati tendaji ya konferensi kamati tendaji ya sinodi.Baraza la saketi na baraza la kanisa kuhakikisha kuwa wanaweka mpango na shughuli na bajeti kuwahudumia kwa haki wahitaji ambao ni watu wasio nauwezo kiuchumi,kijamii na kimaumbile wasioweza kumudu maisha nao ni watoto yatima wajane,watoto walio katika mazingira magumu na wajane.

## IBARA YA 32: KURUGENZI YA RASILIMALI WATU UTAWALA NA UONGOZI

A. Kazi ya rasilimali watu ,utawala na uongozi
1. Kuratibu mpango ya muda mrefu na mfupi na program za kazi za mafuzo kwa ajili ya kuidhinisha na kusimamia utekelezaji wake
2. Kubuni na kusimamia utekelezaji wa uboreshaji wa watumishi,sheria na teknolojia
3. Kutoa taarifa ya utekelezaji wa program zake katika kamati tendaji ya konferensi
4. Kutathmini uendeshaji wa program zake
5. Kushauriana na katibu mkuu na menejiment namna bora ya kuendesha mipango yake ya kiuongozi na kiutawala.
6. Kufanya kazi itakayopangiwa na kamati tendaji ya konferensi

B. Kamati za kurugenzi (Idara zitaundwa kama ifutavyo:;-
a. Mwenye wa bodi au kamati
b. Mkuu wa idara (Katibu wa bodi au kamati)
c. Wajumbe wa bodi au kamati ya kurugenzi au idara kati ya wanne (4) hadi kumi (10)kutegemea ukubwa wa kurugenzi/idara

C. Kazi za Mkuu wa Kuriugenzi/Idara
a. Kusimamia kazi za siku kwa siku za kurugenzi/idara
b. Kusimamia utekelezaji wa maono na utume wa kanisa katika kurugenzi/idara
c. Kutekeleza mpango kazi wa kurugenzi/idara
d. Kutoa taarifa za kazi za kurugenzi/idara kwa katibu mkuu

# SEHEMU YA NANE: FEDHA

### IBARA YA 33: FEDHA, VYANZO VYA MAPATO NA MATUMIZI

1. Methodist church in Tanzania MCT linafundisha kuwazoesha waumini na wanafunzi wake kuwa wanapaswa kumheshimu Mungu kwa matoleo ya mali zao kadri Mungu atakavyowabariki ili injili itangazwe pote kwa kila mtu kufuatana na maandiko matakatifu (**Mithali,3:9,Malaki 3:10)**
   A. Vyanzo vya mapato vimeainishwa kwenye katiba ya MCT Fungu la VIII toleo la juni 2023 uk 127
      i.Zaka
      ii. Sadaka mbali mbali
      iii.Ada ya mwaka ya mkristo
      iv.Shukrani
      v.Malimbuko
      vi.Mavuno
      Viii.Miradi mbali mbali ya kanisa
      Ix.Mikopo kutoka taasisi na Asasi za kifedha
      x. Misaada ya ufadhili kutoka ndani na nje ya Nchi
      Xi.Vyanzo vingine vya mapato halali vitakavyopendekezwa na kamati tendaji ya konfaransa na kuidhinishwa na mkutano mkuu wa konfaransa.
   B. Kanauni hizi zinaelekeza kuwa matumizi na mapato yazingatie sera na usimamizi wa fedha na mali za MCT
   C. Kanuni hizi zinaagiza kuwa kila ngazi ya MCT inatakiwa kufungua akaunti benki ya kanisa na kutumia ipasavyo
   D. Kanuni hizi zinaagiza kuwepo na utunzaji wa kumbukumbu sahihi za mapato na matumizi ya mali za kanisa taarifa zitolewe katika malaka husika kwa mujibu wa sera za usimamaizi wa fedha na mali za MCT.
   E. Kanuni hizi zinaagiza waumini wa MCT kutoa sadaka na michango ya fedha na mali kwa wakati wa ibada na matukio mbalimbali ya kijamii yanayoambatana na ibada ikiwa ni sehemu ya wajibu wa waumini kutokana na sera ya usimamizi wa fedha.
   F. Kanuni hizi zinaagiza kuwa fedha na mali za kanisa zinapatikana kutoka kwa wadau au wafadhili mbalimbali zitaingizwa katika akaunti na kumbukumbu za kanisa kwa mujibu wa taratibu za fedha na matumizi yake na mali za kanisa,
   G. Kanuni hizi zinaagiza kuwa Mali za kanisa lazima ziorodheshwe na zisajiliwe kwa jina la kanisa la Methodist church in Tanzania (MCT) katika ngazi husika.

H. Inapobidi kukodisha,kuingia ubia kuuza hisa au kuingia mkataba katika umiliki na uendeshaji wa mali na huduma za MCT .Kanuni hizi zinaagiza viongozi husika kufuata utaratibu wa vikao husika yenye idhini vya ngazi husika ( Bodi ya wadhamini iliyosajiliwa) kamati tendaji,Bodi ya utawala kwa ajili ya kutoa kibali au ruhusa ya kukodisha au kuingia ubia au kuuza hisa au kuingia mkataba wa wazi na wahalali kwa mujibu wa katiba ya MCT na sera ya usimamizi wa feha na mali za MCT kinyume cha hapo kanuni hizi zinahesabu kuwa tukio hilo ni matumizi mabaya ya madaraka na wizi ambalo linahitajika kuchukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria inavyostahili

I. Kanuni hizi zinaagiza viongozi wa ngazi zote za kanisa kutambua na kutekeleza kanuni za kanisa miongozo mbalimbali ya kifedha zitolewazo na Jamhuri ya muungano wa Tanzania katika kupata na kutumia mapato yake.

2. Kutakuwa na kamati ya fedha katika kila ngazi husika :″
   A. Konferensi
   B. Sinodi
   C. Saketi
   D. Kanisa la mahali

# SEHEMEU YA TISA: NDOA

## IBARA YA 34: NDOA ZA KIKRISTO

1. Kanuni hizi inaelekeza kuwa katika kanisa la MCT tunaamini na kukiri kuwa ni Mungu mwenyezi aliyeanzisha ndoa na kufanya familia alipowaunganisha wanadamu wa kwanza yaani Adam na Hawa ( **Mwz1:27-28,Mwz 2:18-25**) vile vile tunaamini ndoa ni muunganiko/makubaliano ya hiari kati mke mmoja na mme mmoja wala si mme na mme au mke na mke kwa maisha yao yote.Isipokuwa kama ndoa hiyo itafika ukomo kwa mujibu wa sheria za Jamhuri wa muungano wa Tanzania inayotumika .Hata hivyo,kanuni hizi zinatambua uhalali wa ndoa ya kikristo kama inavyofafanua katika taratibu za ibada za MCT
2. Kanisa halitambui ndoa za jinsia moja (**Wal 18:22,20:13**)
3. Kanuni hizi zinaweka msisitizo kuwa ndoa ilioyofungwa madhabahuni ni ndoa ya kudumu kwa maisha yote ya wana ndoa kuwa kilichounganisha na

Mungu mwanadamu asikitenganishe (**Mathayo 19:6**) waumini wote ambao hawakufunga ndoa madhabahuni, wabariki ndoa zao kwa mujibu wa taratibu za ibada za MCT. Unaotumika.

4. Kwa kutambua kuwa maisha ya ndoa yanaweza kuwa na changamoto mbalimbali kanuni hizi zinaelekeza kuwa mashauri yahusuyo ndoa yatatuliwe ndani ya mfumo wa kanisa kabla ya kwenda katika mfumo wa vyombo vya sheria.
5. Kanuni hizi zinaagiza utekelezaji wa katiba ya MCT iliyofanyiwa maboresho Juni 2023 kuwa viongozi wote ndani ya MCT ambao ni wanandoa wanapaswa kuwa na ndoa ya kikristo kila mwenye cheti cha ndoa apeleke nakala ya cheti cha ndoa kwa mchungaji kwa ajili ya kumbukumbu.
6. Kanuni hizi zinaelekeza kuwa endapo itabainika na mamlaka ya kinidhamu katika ngazi husika ya MCT kuwa mwenza wa muumini au kiongozi wa kanisa la MCT ndiye amekengeuka na kutodumisha /kuheshimu nadhiri ya ndoa yao na au kusababisha ukomo wa ndoa kisheria pasipo muumini/kiongozi kusababisha ukomo wa ndoa kisheria hatachukuliwa sheria zozote za kinidhamu na hivyo, ataendelea kuwa na haki na hadhi yake ya muumini/kiongozi.Na kama ndoa yao imefika ukomo kwa mujibu wa sheria za Nchi.  Muumini/kiongozi husika apewe ushauri nasaha na atakuwa huru kuoa/kuolewa katika ndoa takatifu mbele ya madhabahu.
7. Kwa kuwa katiba ya MCT haipingani na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kanuni hizi zinaagiza kuwa ndoa zifungishwe na Askofu na mchungaji mwenye  leseni hai na wala si vinginevyo: Na kwamba waumini na viongozi wa kanisa wataheshimu maamuzi ya mahakama ya juu ya ukomo wa ndoa.

## SEHEMU YA KUMI: KUTATUA MIGOGORO

### IBARA YA 35: TARATIBU ZA KUTATUA MIGOGORO

A: taratibu za kutatua migogoro

B: Kusimamishwa nakuondolewa katika utumishi

Kanuni hizi zinafafanua kuwa kwa mujibu wa katiba ya MCT .toleo la Juni 2023 ukurasa 140 na 141 inaeleza kuwa migogoro inapotokea kuna njia ya kuitatua na kupata suluhisho

## IBARA YA 36: KUSIMAMISHWA NA KUONDOLEWA UTUMISHI

1. Maaskofu wanaokiuka imani,miongozo na sheria za MCT watapewa nafasi ya kusikilizwa na kufutiwa mashitaka,kuonywa,kusimamishwa au kuondolewa katika nafasi zao kutokana na uamzi ndani ya kanisa kwa kuzingatia utovu wa nidhamu,makosa na dhambi walizotenda kwa mujibu wa ibara ya 26 na kanuni za uendeshaji wa MCT
2. Wachungaji nawainjilisti watapita ngazi ya saketi na sinodi na mapendekezo yatapelekwa kwenye kamati tendaji ya nkonferensi kwa uamzi kisha kupeleka baraza la maaskofu utakuwa wa mwisho na Askofu mkuu atatoa taarifa kwenye mkutano mkuu wa MCT.
3. Watumishi wa kuajiriwa kwa mujibu wa sheria za kazi watafuata utaratibu wa kawaida wa kazi na ajira.

## SEHENMU YA KUMI NA MOJA: MAREKEBISHO YA KANUNI NA KATIBA

### IBARA YA 37: MAREKEBISHO YA KANUNI NA KATIBA

A. Kanuni hii inaweza kurekebishwa endapo litapatikana Neno lolote la kuongeza ,kubadilishwa au kufutwa
B. Uteuzi wa kamati ya marekebisho ya katiba na kanuni watateuliwa na kamati tendaji ya konferensi
C. Sifa za wajumbe wa kamati ya kanuni/katiba zitahusisha ubobezi katika maswala ya sheria na utawala na miundo, fedha, uchumi, mipango, uongozi na theolojia.
D. Idadi ya wajumbe wa kamati ya kanuni/katiba haitazidi watu 7 akiwemo mweneyekiti na katibu.

### IBARA YA 38: UTEUZI WA WAJUMBE WA KAMATI YA KANUNI

Rejea katiba ya MCT iliyofanyiwa maboresho juni 2023 ukurasa wa 142,143 na 144.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI: KUVUNJWA KWA KANISA

### IBARA YA 39: UTARATIBU WA KUVUNJWA KWA KANISA

Kanuni ya kuvunjwa kwa kanisa kwa mujibu wa katiba utaratibu wa kuvunjwa kwa kanisa rejea katika katiba ya MCT toleo la juni 2023 ukurasa 146 kifungu cha 1, 2, na 3

## SEHEMU YA KUMI NA TATU: MUUNDO WA MCT

### IBARA YA 40 MUUNDO WA KANISA.


Kutokana na muundo wa MCT anagalia ukurasa wa 59 na 60 chati za michoro


## SEHEMEU YA KUMI NA NNE: MAAFIKIANO

### IBARA YA 41: MAAFIKIANO


Sisi washiriki halisi wa Methodist church in Tanzania (MCT) tumesajiliwa kama kanisa na wizara ya mambo ya ndani ya Nchi kwa usajili wa **S.A 6945** kwa lengo kuu la kumwabudu Mungu na kujifunza Neno la Mungu, kushirikiana na Neno la Mungu kama ilivyo katika Biblia. Tunajifunza na kupokea kanuni hizi kwa matumizi katika kuendeleza neno la Mungu na kulinda kazi zetu zote kama watu wanaomwabudu na kukubaliana na matakwa ya kibiblia,utekelezaji utafanyika kama ambavyo kamati tendaji ya konferensi inaelekeza na kwa mujibu wa kanuni za uendeshaji.

**<u>MUUNDO WA KANISA</u>**






**MUUNDO WA SINODI**


MKUTANO MKUU WA
ASKOFU WA SINODI
KAMATI TENDAJI
KATIBU MKUU
MHASIBU WA SINODI
IDARA MBALIMBALI ZA
MCHUNGAJI KIONGOZI
KATIBU WA SAKETI
MHASIBU WA SAKETI
MCHUNGAJI
BARAZA LA SKETI
MWINJILISTI
MZEE WA KANISA
BARAZA LA KANISA
MHASIBU WA KANISA
SHEMASI

WAUMINI WA KANISA